# Nipashe

Jumanne Mei 4, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580570

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




**Spika** aanika dosari barua ya CHADEMA kutimua wabunge 19

UKURASA 3

**Kontena** 500 zatelekezwa bandarini

UKURASA 3



**Messi afunga bao la 50 la mpira uliokufa Barca**

UKURASA 20

# Utouh: Mikopo ya vyuo vikuu ifutwe

UKURASA 2





Mhariri Mtendaji wa gazeti la The Guardian, Wallace Maugo, akiwaeleza mabalozi wa Uingereza, David Concar (kushoto) na Balozi wa Canada, Pamela O'Donell, jinsi chumba cha habari kinavyofanyakazi walipotembelea vyombo vya habari vya IPP, Mikocheni jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa The Guardian Ltd, Joyce Luhanga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mabalozi waona mwanga uhuru wa habari Tanzania

UK. 2

## Wafariki dunia kwa kufukiwa na kifusi

UKURASA 3

**MICHEZO** KOCHA WA YANGA AAHIDI 3 ZA SIMBA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Utouh: Mikopo ya vyuo vikuu ifutwe

Na Sanula Athanas

MWAKA 1994/95, serikali ilianza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu na miaka 10 baadaye, yaani mwaka 2004 utoaji wa mikopo hiyo ukachagizwa zaidi na kuanzishwa kwa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB).

Hata hivyo, utoaji wa mikopo hiyo umekumbwa na malalamiko kutoka kwa wadau ikiwa ni pamoja na kuwapo kwa kile kinachotajwa kuwa uonevu katika marejesho.

Vilevile, zipo hoja za matumizi mabaya ya fedha za bodi hiyo zilizoibuliwa na vyombo vya ukaguzi ikiwamo Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Kwa kurejea machache, PAC ilibaini mamilioni ya HESLB kutumiwa na maofisa wake kulipana posho mbalimbali ikiwamo ya ukarimu, huku Ripoti mpya CAG ikibainisha wadaiwa sugu 128,278 hawajulikani waliko na wanatakiwa kurejesha Sh. bilioni 706.7 walizokopeshwa.

Wakati hali ikiwa hivyo, aliyekuwa CAG, Ludovick Utouh, anaishauri serikali kuifuta mikopo hiyo.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki iliyopita, Utouh alisema anaona kuna haja kuachana na utoaji wa mikopo ya elimu ya juu kwa kuwa ufanisi umekosekana katika marejesho huku kukiwapo taarifa za uonevu katika kurejesha mikopo hiyo.

Utouh ambaye kwa sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, alisema elimu ni miongoni mwa huduma za msingi ambazo serikali inapaswa kuzitoa kwa wananchi wake, hivyo siyo haki wananchi kukopeshwa fedha ili wapate haki yao.

"Niseme tu kwamba mkopo ni pesa ambayo unaipokea ili baadaye uilipe, lakini tulisema tunakopesha watu wasome, waajiriwe na kupitia mshahara wao wa kuajiriwa warudishe deni.

"Sasa tunasomesha watu wanahitimu lakini hawana ajira, ndio maana CAG anasema kuna wadaiwa sugu 128,000 na watu hao wakati mwingine hata kuwapata katika mifumo maalum inakuwa ni shida. "Kwa hiyo, mimi ninafikiri tunatakiwa kurudia kufikiria yale mawazo ya kukopesha mtu asome, ahitimu, ajiriwe, kupitia mshahara alipe deni.

"Sasa, kwenye hali yetu hii ambayo hakuna ajira, tutawezaje kurudisha gharama hizo? Tufike mahali tufikirie tena hii mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

"Watu wanasoma kupitia mikopo lakini hawajaajiriwa, ni vipi watarudisha? Kuwe na sheria ya kusema kuwa huyo mtu akimaliza masomo yake bila kupata ajira kwa kipindi fulani nini kifanyike, kuliko kuripoti kwenye vitabu kusema bodi ya mikopo inadai kiasi kikubwa wakati tunajua uwezekano wa kurudisha ni sifuri.

"Sisi tuliosoma zamani tulikuwa hatulipi, tulipewa hadi fedha za usafiri (nauli) lakini wakati huo tulikuwa wachache na vyuo vilikuwa vichache.

"Suala la afya, elimu na maji ni jukumu kwa kuwa ndiyo huduma kuu zinazopaswa kutolewa na serikali," Utouh alifafanua.

Takwimu za HESLB za mwaka 2019, zilibainisha kuwa kati ya Watanzania 479,779 waliopatiwa mikopo hiyo tangu serikali ilipoanza kuitoa mwaka 1994/15, ni wanufaika 11,214, sawa na asilimia 2.3 waliofanikiwa kumaliza kulipa madeni yao.

Deni kuongezeka kwa asilimia sita kila mwaka, kumekuwa kukitajwa kuwa kiini cha wanufaika wengi wa mikopo hiyo kushindwa kumaliza kulipa madeni yao.

Katika hotuba yake jijini Mwanza wakati wa sherehe za Siku ya Wafanyakazi Mei Mosi mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alitangaza kuifuta 'riba' hiyo iliyolalamikiwa kwa muda mrefu.



Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Rais mstaafu wa Nigeria, Jenerali Olesegun Obasanjo, aliyemtembelea Ikulu Chamwino mjini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Samia akutana na Jenerali Obasanjo

Na Mwandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan, amekutana na kufanya mazungumzo na Rais Mstaafu wa Nigeria, Jenerali Olusegun Obasanjo.

Mazungumzo hayo yalifanyika jana Ikulu Chamwino jijini Dodoma, ambapo Jenerali Obasanjo alitoa salamu zake za rambirambi kwa Rais Samia kufuatia vifo vya waliokuwa marais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Benjamin Mkapa na Hayati Dk. John Magufuli, waliofariki dunia Julai 23 , 2020 na Machi 17, 2021.

Rais Mstaafu Obasanjo alimpongeza Rais Samia kwa kupokea kijiti cha kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na amemtakia heri katika majukumu yake. Aidha, katika mazungumzo hayo viongozi hao walizungumzia hali ya usalama barani Afrika na umuhimu wa wakuu wa nchi kujadiliana na kutafuta suluhisho la migogoro hiyo, ambayo inasababisha vifo vya watu wasio na hatia hasa wanawake na watoto.

Pia, viongozi hao walizungumzia masuala ya maendeleo hasa katika uchumi na kusisitiza umuhimu wa nchi za Afrika kuongeza ushirikiano na kuondoa vikwazo vya biashara na uwekezaji.

## Mabalozi wasifu mabadiliko uhuru vyombo vya habari

Na Christina Mwakangale

MABALOZI wa Canada na Uingereza wanaoziwakilisha nchi zao nchini, wamesema wanafurahishwa na mabadiliko yanayoanza kuonekana nchini kwa uhuru wa vyombo vya habari na kusisitiza ubora wa habari na zinazoaminika ni muhimu ili kujenga imani kwa wananchi.

Balozi wa Canada nchini Tanzania, Pamela O'Donnell, akizungumza jana baada ya kufanya ziara katika vyombo vya habari vya IPP, Mikocheni, jijini Dar es Salaam, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha kuanza vyema na tayari watu wana utayari wa kutoa mchango na maoni yao katika maendeleo ya nchi na serikali yao.

Katika ziara hiyo balozi O'Donnell ambaye aliambatana na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, David Concar William, walilenga kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani inayofanyika Mei 3, kila mwaka.

Balozi O'Donnell alisema uhuru wa vyombo vya habari ni muhimu kwa kuwa hufanya vyombo hivyo kuibua na kuripoti kwa uhuru, usahihi na kuleta mabadiliko kwenye jamii ikiwamo serikali kuchukua hatua.

"Ukiwa na taasisi zisizo za kiraia huru, vyombo vya habari huru, wakiungana wanasaidia kuibua masuala mbalimbali na serikali kuchukua hatua," alisema Balozi O'Donnell.

Alisema katika kuhakikisha kuna uhuru huo, Canada inaungana na nchi nyingine duniani kupitia miradi mbalimbali kuviwezesha vyombo vya habari kuongeza ubora wa habari zao.

Vilevile, Balozi Concar, alisema uhuru wa vyombo vya habari ikiwamo kuripoti taarifa kwa usahihi na zinazotoa haki pande zote, kunakifanya chombo kuaminiwa kwenye jamii, huku akivipongeza vyombo vya habari vya IPP kwa kutoa hababari zenye ubora.

"Hatua nyingi duniani huchukuliwa baada ya chombo cha habari kuripoti. Uhuru kwa vyombo vya habari ni muhimu kama ilivyo umuhimu wa kutumia hewa ya Oksijeni. Tunafurahi kuwa hapa (IPP) leo na kuona mkifanyakazi kubwa na kutumia wafanyakazi wenye weledi," Balozi Concar.

Mkurugenzi Mtendaji wa ITV/ Radio One, Joyce Mhaville, alisema katika kufanikisha ubora wa habari, kila mmoja hufanya majukumu yake ipasavyo kuanzia kuitafuta habari hadi inapokwenda hewani.

Mkuu wa idara ya habari ITV, Steven Chuwa, alisema kukua kwa teknolojia katika vyombo vya habari kumeleta changamoto, kutokana na kuibuka kwa waandishi ambao hawajasomea hata uandishi wa habari na kutumia mitandao ya kijamii vibaya.

HABARI KITAIFA

# Spika ataja kasoro barua ya CHADEMA wabunge 19

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amewaondoa hofu wabunge 19 wa viti maalum kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), akiwataka kuendelea kuchapa kazi kwa kuwa wako kwenye mikono salama.

Kiongozi huyo wa Bunge alilazimika kutoa ufafanuzi huo bungeni jijini hapa jana baada ya kuwapo kwa shinikizo kutoka uongozi wa juu wa CHADEMA unamwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuingilia kati sakata hilo.

Kwa mujibu wa CHADEMA, wabunge hao 19 wakiongozwa na aliyekuwa Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake CHADEMA (BAWACHA), Halima Mdee, walifukuzwa uanachama Novemba mwaka jana, baada ya kwenda bungeni kuapishwa pasipo idhini ya chama.

Wabunge hao ni Agnesta Kaiza, Nusrat Hanje, Asia Mohamed, Felister Njau, Stela Fiyao, Halima Mdee, Grace Tendega, Esther Matiko, Cecilia Paresso, Esther Bulaya, Jesca Kishoa, Hawa Mwaifunga, Tunza Malapo, Naghenjwa Kaboyoka, Sophia Mwakagenda, Kunti Majala, Anatropia Theonest, Salome Makamba na Conchesta Rwamlaza.

Akitolea ufafanuzi wa suala hilo jana bungeni, Spika Ndugai alisema kuna taratibu za kufuatwa ili mbunge afukuzwe. Spika Ndugai alisema: "Niwaambie vyama vya siasa mimi ni Spika mzoefu, nimekuwa hapa bungeni miaka 20 sasa ninaelekea 25, nina uzoefu wa kutosha, wapo watu wanaopiga kelele Ndugai anavunja katiba, yaani hawaelewi watendalo kabisa yaani.

"Katibu Mkuu wa chama chochote kile akiniandikia jambo lenye mgogoro ambao unasababisha mambo ya kikatiba, mgogoro unaotoka kwako msiniandikie kipeperushi... Eti 'mimi fulani ninasema kwamba Spika chukua hatua fukuza fulani na fulani'.

"Kazi yangu mojawapo ni kulinda wabunge, mkiruhusu hayo mtapata tabu waheshimiwa. Katibu Mkuu wa chama chochote huko ulikotoka ananiandikia kipeperushi halafu mimi (Spika) nichukue hatua ya kuwafukuza wabunge, haiendi hivyo.

"Aandike barua na kuambatanisha na katiba yake ya chama chake, kwa sababu mimi (Spika) siwezi kujua katiba ya vyama, anachotakiwa kufanya ni aambatanishe muhtasari wa kikao kilichofanya uamuzi wa kuwafukuza.

"Kwa sababu inawezekana huyo Katibu Mkuu kaamka tu kaandika barua halafu na mimi ninakurupuka ninachukua hatua ya kuwafukuza, nitakuwa ni Spika au kitu cha ajabu?

"Aandike barua rasmi niipitie, niwape wataalamu wa sheria maana ninao wengi, wataitathimini kama iko sawa, wataangalia wajumbe wa kikao cha kamati kuu iliyokaa kuwafukuza hao wabunge ndiyo wajumbe halisi? Kisha nitamuuliza Msajili wa Vyama Vya Siasa.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akisalimiana na Mufti na Sheikh Mkuu wa Tanzania, Abubakar Zubeir, alipowasili kwenye ukumbi wa Diamond Jublee jijini Dar es Salaam kuwa mgeni rasmi katika fainali za mashindano ya kimataifa ya Quran Tukufu, juzi. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge. **PICHA: OWM**

# Kontena 500 zatelekezwa bandarini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, ameagiza kukamatwa kwa Kaissy, Mkurugenzi wa Kampuni ya Seif for Tobacco Trading Co. Ltd aliyeingiza nchini kontena zaidi ya 500 zenye malighafi ya Molasesi iliyoharibika na kuzitelekeza katika Bandari ya Dar es Salaam.

Jafo alitoa agizo hilo jana baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika Bandari ya Dar es Salaam na kushuhudia kontena hizo zikiwa zimetelekezwa bandarini huko na zingine kutawanywa katika baadhi ya bandari kavu jijini Dar es Salaam.

Alisema kamwe Tanzania haiwezi kugeuzwa kuwa dampo kwa kuruhusu kuingizwa bidhaa kutoka nje ya nchi ambazo muda wake wa matumizi kuisha.

Ilidaiwa kuwa mfanyabiashara huyo aliyetambulika kwa jina moja la Kaissy, aliingia nchini kwa hati ya utembezi (tourist) na baadaye kupatiwa kibali cha uwekezaji kupitia EPZA kilichomruhusu kuwekeza katika uzalishaji wa shisha, kibali ambacho kilifutwa baada ya kugundulika kuwapo udanganyifu mkubwa kuhusu uwekezaji wake.

Waziri Jafo alimwagiza Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa na Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samwel Gwamaka, kufanya ukaguzi katika bandari kavu zote nchini kubaini bidhaa zilizoingizwa nchini zikiwa zimeisha muda wake wa matumizi ambazo zimetelekezwa kwa lengo la kuzitupa nchini na kuchukua hatua za kisheria.

Jafo pia aliagiza NEMC, TBS na Mamlaka ya Bandari ndani ya siku tatu kuwasilisha taarifa ya kina kuhusu mwekezaji huyo na idadi kamili ya kontena zilizoingizwa nchini na mfanyabiashara huyo.

Waziri Jafo pia alitembelea bomba za kusafirishia mafuta kutoka kwenye meli na kubaini uvujaji wa mafuta katika mabomba hayo unaosabishwa na uchakavu wa mitambo hiyo.

Kutokana na hali hiyo, Jafo aliagiza hatua za haraka kuchukuliwa kudhibiti uchafuzi wa mazingira.

## Kifusi chaua watu watatu

**Na Allan Isack,** ARUMERU

WATU watatu wamefariki dunia na wengine watatu kujeruhiwa baada ya kufukiwa na kifusi katika machimbo ya changarawe, maarufu moramu, yaliyoko Kijiji cha Engorora wilayani Arumeru mkoani Arusha.

Taarifa zilizothibitishwa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, zilibainisha kuwa watu hao walifukiwa na kifusi hicho jana asubuhi katika machimbo hayo wakati wakichimba changarawe.

"Ni kweli hilo tukio limetokea leo (jana) asubuhi majira ya saa tatu. Kulikuwa na wanakijiji sita wanachimba moramu na wakati wakiendelea na shughuli hiyo, kifusi kilianguka na watatu wakafa papo hapo.

"Wengine watatu walinusurika ingawa wameumia vibaya. Kazi ya kuwaokoa watu hao ilifanywa na wanakijiji wenzao na baada ya kuokolewa walikimbizwa kupata tiba ya awali, Zahanati ya Kisongo," alisema.

Aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Nurdin Rajabu (29), Idd Hussein (26) na Bonkila Martine (27), wote wakazi wa Ngorbobo, Wilaya ya Arumeru.

"Ripoti ya awali niliyopokea inaonyesha kwamba waliojeruhiwa ni Evarist Martin (25), Haruna Mbasha (32), Elias Kigeso, wote wakazi wa Ngorbobo, Wilaya ya Arumeru," alibainisha.

Kwa mujibu wa Kamanda Masejo, miili ya watu hao watatu imehifadhiwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Arusha (Mount Meru). Vilevile, alisema majeruhi walipatiwa matibabu katika Kituo cha Afya cha Kisongo na baada ya muda mfupi hali zao za kiafya ziliimarika na waliruhusika kurejea nyumbani.

**RC KIMANTA**

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Iddy Kimanta, ambaye alizuru eneo hilo la machimbo baada ya kutokea kwa ajali, alisema tayari ameelekeza maofisa madini kufanya upembuzi yakinifu kama machimbo hayo yanastahili kuendelea kufanya kazi au la.

"Huenda machimbo haya ya Engorora hayakuzingatia utaratibu wa kiusalama, lakini baada ya wataalamu kuyakagua, watatushauri nini kifanyike," alisema.

**Huenda machimbo haya ya Engorora hayakuzingatia utaratibu wa kiusalama, lakini baada ya wataalamu kuyakagua, watatushauri nini kifanyike.**

HABARI KITAIFA

# Watanzania 57 waukana uraia

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi mwaka huu, Watanzania 57 waliukana uraia na kupata uraia wa mataifa mengine.

Kadhalika, amesema hadi kufikia Machi, mwaka huu idadi ya vitambulisho vilivyozalishwa na kusambazwa ni 7,028,567 katika wilaya 34 za Tanzania Bara na Zanzibar.

Alitoa taarifa hiyo jana wakati akiwasilisha bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa wizara yake kwa mwaka 2021/22, akiomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 939.

Simbachawene alisema Watanzania hao waliopatiwa uraia katika mataifa ya Afrika Kusini (1), Australia (2), Austria (1), Botswana (3), Canada (9), India (5), Italia (2), Kenya (3), Lebanon (1), Marekani (10), Namibia (1), Uholanzi (1), Oman (1), Rwanda (2), Uganda (1), Uingereza (5), Ujerumani (8) na Yemen (1).

Alisema idadi ya wageni walioomba na kupewa uraia wa Tanzania katika kipindi cha Julai, 2020 hadi Machi, 2021 walikuwa ni 52.

Alisema wageni hao ni kutoka mataifa ya Cameroon (1), Ghana (1), India (20), Kenya (3), Lebanon (2), Pakistani (4), Somalia (2), Uganda (1), Uingereza (2), Uturuki (1), Yemeni (12) na wasiokuwa na utaifa (3).

### HATI ZA KUSAFIRIA

Mbali na hilo, Simbachawene alisema katika kipindi hicho, Idara ya Uhamiaji ilitoa hati za kusafiria 54,072 kwa Watanzania waliotaka kusafiri nje ya nchi.

Alisema kati ya hizo, hati za kusafiria za Kidiplomasia ni 133, Kiutumishi 22 na za kawaida ni 53,917. Vilevile, jumla ya Hati za Safari za Dharura 164,506 zilitolewa.

Aidha, alisema Watanzania 310 waliokwenda nje ya nchi kinyume na taratibu za uhamiaji walirudishwa nchini

Kuhusu Visa, Simbachawene alisema zilitolewa 224,544 hadi kufikia Machi, mwaka huu, kwamba visa za matembezi ni 203,324, biashara 20,929 na kidiplomasia 291 ikilinganishwa na Visa 337,411 zilizotolewa kwa mwaka 2019/2020.

Alisema vibali vya ukaazi 12,676 vilitolewa kwa wageni walioingia nchini katika kipindi hicho.

### VIBALI VYA UKAAZI

Kuhusu udhibiti wa uingiaji, ukaaji na utokaji wa wageni, Simbachawene alisema Idara ya Uhamiaji ilisimamia uingiaji wa wageni 511,243 nchini ikilinganishwa na wageni 1,158,022 walioingia katika kipindi kama hicho mwaka 2019/2020.

Alisema wageni 421,687 walitoka nchini ikilinganishwa wageni 1,048,149 waliotoka kwa mwaka 2019/2020, kwamba katika kipindi hicho wageni 201 walizuiliwa kuingia nchini kutokana na sababu za kiusalama na kutokidhi vigezo vya kiuhamiaji.

"Idadi ya wageni walioingia na kutoka nchini kwa mwaka 2020/2021 imepungua ikilinganishwa na mwaka 2019/2020 kutokana na ugonjwa wa homa ya mapafu," alisema Simbachawene.

### VITAMBULISHO

Kuhusu Vitambulisho vya Taifa, Simbachawene alisema hadi kufikia Machi, mwaka huu usajili wa wananchi umeongezeka na kufikia watu 22,345,948 ikilinganishwa na lengo la kusajili watu 25,237,954.

Alisema wageni wakaazi 32,170 na wakimbizi 213,251 wamesajiliwa, namba za utambulisho 18,762,822 zimezalishwa na kugawiwa kwa wananchi.

"NIDA imezalisha na kusambaza vitambulisho 925,342, hivyo kufanya idadi ya vitambulisho vilivyozalishwa na kusambazwa hadi Machi, 2021 kufikia 7,028,567 katika wilaya 34 za Tanzania Bara na Zanzibar," alisema Simbachawene.

Alisema kazi ya uzalishaji vitambulisho katika wilaya 116 zilizobaki inaendelea na inatarajiwa hadi kufikia Julai, 2021 watu wote wenye namba za utambulisho watapata vitambulisho.

Alisema namba za utambulisho 13,932,455 zilitumika katika usajili wa simu kwa lengo la kuimarisha usalama.

Alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, NIDA itaendelea na zoezi la usajili na utambuzi katika wilaya na mikoa yote nchini, watu 1,438,735 wanatarajiwa kusajiliwa.

### USAFIRISHAJI BINADAMU

Kuhusu biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu, Simbachawene alisema serikali imefanikiwa kuwaokoa na kuwasaidia watu 165 waliokuwa wanatumikishwa kufanya kazi kama vile kuomba mitaani, kazi za majumbani, kutumikishwa kingono, kazi ngumu kwenye mashamba na migodi.

Alisema kati yao watu 163 walikuwa wanatumikishwa hapa nchini, wawili walikuwa wanatumikishwa Iraq na Malaysia.



Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii, Mwanaidi Ali Khamis, akipata maelezo ya miradi ya ujenzi wa mabweni ya wasichana na kumbi za mihadhara kutoka kwa Naibu Mkuu wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii, Utawala na Fedha, Janeth Zemba, wakati alipotembelea taasisi hiyo. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Rais Samia atengua uteuzi viongozi 3

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ametengua uteuzi wa viongozi watatu.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Kattanga, ilieleza kuwa uteuzi wa viongozi hao umetenguliwa kuanzia Aprili 30, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, Rais Samia ametengua uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Wakala wa Meli Tanzania (TASAC), Prof. Tadeo Andrew Satta.

Sambamba na hatua hiyo, Rais Samia pia ametengua uteuzi wa wajumbe sita wa Bodi ya TASAC.

Pia Rais Samia ametengua uteuzi wa Posta Masta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania, Hassan Mwang'ombe.

Kadhalika, Rais Samia ametengua uteuzi wa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Posta Tanzania, Dk. Harun Kondo.

Sambamba na hatua hiyo, Rais Samia vilevile amevunja Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Posta Tanzania.

Taarifa iliongeza kwamba uteuzi wa viongozi watakaoshika nyadhifa hizo utafanywa baadaye.

# Wafuasi CHADEMA waachiwa huru

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Bukoba imemwachia huru aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Bukoba na mgombea ubunge Jimbo la Bukoba Mjini (CHADEMA), Chief Kalumuna na wafuasi wengine sita wa chama hicho waliokuwa wanakabiliwa na mashtaka manane likiwamo la kumjeruhi Mkuu wa Polisi Wilaya ya Bukoba, SSP Babu Sanare.

Akisoma hukumu ya kesi hiyo namba 257 ya mwaka 2020 iliyokuwa inawakabili washtakiwa saba, hakimu wa mahakama hiyo, Joseph Ruambano, alitaja mashtaka mengine yaliyokuwa yakiwakabili washakiwa hao ni kusababisha vurugu na uharibifu wa mali.

Hakimu Ruambano alisema kuwa upande wa Jamuhuri walikuwa na mashahidi sita ambao walitoa ushahidi dhidi ya washtakiwa hao wakidai walitenda makosa hayo katika Uwanja wa Kaitaba kulipokuwa kunafanyika uapisho wa mawakala, wagombea wa udiwani na ubunge katika Jimbo la Bukoba Mjini.

Pamoja na washtakiwa hao kukubali kuwapo eneo la tukio siku hiyo, walikana kutenda makosa hayo kwa kuwa siku hiyo Uwanja wa Kaitaba kulikuwapo michezo ya wanafunzi, na timu ya Kagera Sugar ikifanya mazoezi, suala ambalo upande wa Jamhuri ulishindwa kuthibitisha kuwa wafuasi wa CHADEMA ndiyo waliohusika na tukio hilo.

Hakimu huyo pia alisema shahidi namba nne kwa upande wa Jamhuri SSP Babu Sanare aliyejeruhiwa wakati wa vurugu hizo, alishindwa kuthibitisha kujeruhiwa na mshtakiwa namba nne Audomalius Audax Joseph.

# Wabunge walalamikia vitambulisho vya taifa

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WABUNGE wameilalamikia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kuhusu ucheleweshaji wa utolewaji wa vitambulisho, kwamba wananchi wengi wamekuwa wakiteseka kila siku kufuatilia.

Wamesema kazi ya utolewaji wa vitambulisho hivyo imegubikwa na ubabaishaji, hivyo kusababisha wananchi wengi kukata tamaa.

Waliyasema hayo jana bungeni wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa mwaka 2021/22.

Mbunge wa Viti Maalum, Sophia Mwakagenda, alisema utolewaji wa vitambulisho vya taifa umekuwa wa shida hususani maeneo ya vijijini.

Alisema idadi ya Watanzania waliopata haizidi milioni nane, kwamba serikali imeshatangaza mwisho wa upatikanaji wa vitambulisho hivyo kuwa ni Juni 8, mwaka huu. Wakati idadi kubwa ikiwa imepatiwa namba.

Mwakagenda alisema: "Waziri tuambie mwisho wa changamoto hii ni lini, kwa sababu Watanzania wengi wanateseka kuvipata na ukizingatia wanakosa huduma muhimu kwa sababu hawana vitambulisho."

Naye Mbunge wa Makambako (CCM), Deo Sanga, alisema: "Upatikanaji wa vitambulisho vya taifa umekuwa wa shida, wengi wanaandikisha wanapewa namba tu, wengi wanatoka wilayani wanasumbuliwa kila siku njoo kesho njoo kesho."

Naye Mbunge wa Viti Maalum, Ester Matiko, alisema idadi ya Watanzania waliopata vitambulisho vya taifa ni ndogo kulinganisha na waliopata.

Naye Mbunge wa Kyerwa (CCM), Innocent Bilakwate, alisema wananchi wa jimboni kwake wanakwenda kwenye ofisi za NIDA hawapati vitambulisho wanaambiwa tatizo ni mtandao.

Alisema inaonekana serikali haijajipanga katika ugawaji wa vitambulisho vya taifa, wananchi wanatembea zaidi ya kilometa 30 kufuata vitambulisho lakini hawavipati.



Mwenyekiti mpya wa Chama cha Ushirika cha Msingi Umoja Liwale mkoani Lindi, Hassan Myao, akitoa neno la shukrani kwa wanachama hao (hawapo pichani), mwishoni mwa wiki, baada ya kumchagua kwa kipindi cha miaka mitano ijayo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TEF: Uhuru vyombo vya habari sio wa kuridhisha

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JUKWAA la Wahariri Tanzania (TEF), limesema bado hali ya uhuru wa vyombo vya habari nchini, sio ya kuridhisha kutokana na Tanzania kuporomoka viwango vya kimataifa kutoka nafasi ya 71 mwaka 2016 hadi nafasi ya 124 mwaka 2020.

Licha ya kushuka kwa viwango hivyo, jukwaa hilo limempongeza Rais Samia, kwa kutambua umuhimu wa mchango wa vyombo vya habari, baada ya kuagiza vyombo vilivyokuwa kifungoni vifunguliwe.

Akizungumza jana wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, yaliyofanyika kitaifa jijini Arusha, Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, alisema hotuba ya Rais Samia imeleta nuru, baada ya hotuba yake ya Aprili 6, mwaka huu.

Rais Samia aliagiza kufunguliwa vyombo vya habari vilivyofungiwa zikiwamo televisheni za mtandaoni na kuhakikisha wanafuata kanuni zilizowekwa na serikali.

"Hali hii imetokana na kufungiwa kwa magazeti na kufunguliwa kesi za jinai, badala ya madai kwa baadhi ya vyombo vya habari, kupigwa na kunyang'anywa baadhi ya vifaa vya wanahabari," alisema Balile.

Aidha, alisema ni vyema watawala wakaheshimu uhuru wa habari na kufanya kazi kwa ushirikiano na wanahabari, kwa vile zipo nchi nyingi duniani zimeingia kwenye shida, kwa sababu ya matukio madogo kama yanayotokea nchini.

Kutokana na hali hiyo, TEF imeiomba serikali kufuatilia kwa karibu matukio ya wanaofungia wanahabari na vyombo vya habari ili kuwadhibiti watu wachache wanaoendelea kuharibu dhamira njema ya serikali.

Alitumia maadhimisho hayo, pia kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), kwa kuchukua hatua za haraka kwa askari wa Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) ambao walimpiga na kumnyang'anya vifaa vya kazi mwandishi wa habari, Jose Mikofu, mwezi Aprili mwaka huu.

**BASHUNGWA ATOA MWELEKEO**

Akitoa mwelekeo wa serikali, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, alisema serikali itaendelea kushirikiana na waandishi wa habari pamoja na wadau wa habari nchini, kwa ajili ya kuendelea kuelimisha jamii mambo mbalimbali yenye tija kwa taifa.

"Naomba niwatoe hofu serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, ipo tayari kushirikiana nanyi vizuri, na msiwe na wasiwasi. Hayo yote mnayosema hayatakuwapo na tunakaribisha mazungumzo pale mnapoona hapaendi sawa ili mradi kila mmoja afanye kazi kwa uhuru.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi chache zenye vyombo vingi vya habari barani Afrika, na hiyo inatokana na uhuru wa vyombo vya habari uliopo nchini.

"Mpaka sasa serikali imesajili magazeti 246, televisheni 53, redio 194, redio za mtandaoni 23, blogs 120 na televisheni za mtandaoni 440.

"Hii ni ishara kwamba nchi yetu inathamini na kuenzi vyombo na taaluma ya habari. Hivyo basi, kuhakikisha vyombo vya habari vina hali nzuri kiuchumi na kunakuwapo na uwazi kwenye upatikanaji wa habari, ikiwa pamoja na kusaidia vyombo vya habari vichanga, kwa kuviongezea uwezo kiutendaji."

Katika maadhimisho hayo, Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Tirso Dos Santos, alisema shirika hilo limekuwa likisaidia taaluma ya habari katika nyanja mbalimbali nchini, kwa kuwajengea uwezo wanawake viongozi katika sekta ya habari.

Alisema licha ya kujengea uwezo wanawake, mwaka jana walitumia zaidi ya Sh. milioni 400 kwa ajili ya kununua vifaa vya redio 16 za kijamii nchini lengo likiwa kuhakikisha jamii inapata habari kwa wakati.

# Vigogo CWT kortini tuhuma za ufisadi

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO wawili wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), akiwamo Katibu Mkuu, Deus Seif na Mhazini, Abubakar Allawi, wamefikishwa mahakamani, wakikabiliwa na mashtaka mawili ikiwamo la matumizi mabaya ya madaraka na kijipatia Sh. milioni 13.9 mali ya chama hicho.

Washtakiwa hao wamesomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TUKUKURU), Imani Mitume, ambaye alidai kati ya Oktoba 3 na Novemba 6, 2018, katika ofisi za CWT zilizopo Kinondoni, washtakiwa wakiwa waajiriwa wa chama hicho, walitumia madaraka yao vibaya na kujipatia Sh.13, 930,693.

Shtaka la pili, ilidaiwa siku na mahali pa tukio la kwanza, Seif na Allawi kwa kutumia madaraka yao vibaya na kwa manufaa yao wanadaiwa kuchepusha fedha mali ya CWT.

Upande wa Jamhuri walidia kuwa upelelezi umekamilika.

Mitume alidai kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini(DPP) amewasilisha hati ya kuipa kibali mahakama hiyo kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu Chaungu alisema dhamana ya washtakiwa hao iko wazi kila mshtakiwa anatakiwa kuwasilisha fedha taslimu Sh. milioni 3.4 au mali isiyohamishika yenye thamani hiyo.

Alisema mbali na washtakiwa kuwasilisha fedha hizo, pia wanatakiwa kuwa na mdhamini mmoja kila mshtakiwa watakaotia saini hati ya dhamana ya Sh. milioni 7.

Mshtakiwa Allawi alishindwa kutimiza masharti ya dhamana, huku Seif akipata dhamana na kesi hiyo imeahirishwa hadi Mei 17, 2021 itakapotajwa.

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Upo umuhimu serikali, wanahabari kuzungumza

**APRILI** 16, mwaka huu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, alitoa kauli iliyoleta matumaini makubwa kwa vyombo vya habari, baada ya kuagiza vyombo vya habari vilivyofungiwa vifunguliwe.

Hata hivyo, alivitaka vyombo hivyo vifuate taratibu na sheria katika kufanyakazi zao. Kwa mujibu wa takwimu zilizonukuliwa na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), hali ya uhuru wa vyombo vya habari nchini, sio ya kuridhisha kutokana na kuporomoka viwango vya kimataifa kutoka nafasi ya 71 mwaka 2016 hadi nafasi ya 124 mwaka 2020.

Hali ya kufungiwa kwa baadhi ya magazeti na televisheni mtandao, imekuwa ikilalamikiwa na wadau wa habari kwa kubinywa kwa uhuru wa vyombo vya habari na kunyima wananchi haki ya kupata habari.

Mwenyekiti wa TEF, Deodatus Balile, katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Duniani, yaliyofanyika jana kitaifa jijini Arusha, amempongea Rais Samia kwa hatua yake ya kuagiza vyombo hivyo kufunguliwa kwa kuwa imeleta nuru mpya.

Kufungiwa kwa magazeti na kufunguliwa kesi za jinai, waandishi wa habari kupigwa na kunyang'anywa baadhi ya vifaa vya kazi na wengine kupotea ni matukio ambayo yamekuwa yakilalamikiwa na wadau wa vyombo vya habari kutofanyakazi yao kwa uhuru.

Vyombo vya habari kwa kutoandika habari za kuibua masuala kuleta mabadiliko katika nchini, kulipoteza dhana nzima ya vyombo hivyo katika kuzingatia misingi na weledi wa taaluma yao kuisaidia serikali kutekeleza majukumu yake katika utawala bora.

TEF imeomba watawala kuheshimu uhuru wa habari na kufanya kazi kwa ushirikiano na wanahabari na kufuatilia kwa karibu matukio ya wanaofungia wanahabari na vyombo vyake ili kuwadhibiti watu wachache wanaoendelea kuharibu dhamira njema ya serikali.

Tunaanza kuona matumaini mapya baada ya serikali kupitia Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Innocent Bashungwa, inakaribisha mazungumzo pale vyombo vya habari vinapoona mambo hayaendi sawa ili kila mmoja afanye kazi kwa uhuru.

Na kwamba serikali itaendelea kushirikiana na waandishi wa habari pamoja na wadau wa habari nchini kwa ajili ya kuendelea kuelimisha jamii mambo mbalimbali yenye tija kwa taifa. Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini kutoka Canada, Uingereza na Marekani wamepongeza pia hatua iliyoanza kuoneshwa na Rais Samia katika kuleta mabadiliko ya uhuru wa vyombo vya habari.

Hata hivyo, wamevitaka vyombo vya habari kuandika habari zenye uhakika, kuaminika na zinazotoka haki pande zote ili wananchi waweze kujenga imani kwa vyombo hivyo.

Katika maadhimisho hayo, Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), Tirso Dos Santos, alisema shirika hilo limekuwa likisaidia taaluma ya habari katika nyanja mbalimbali sekta, kwa kuwajengea uwezo wanawake viongozi katika sekta ya habari.

Alisema licha ya kujengea uwezo wanawake, mwaka jana wametumia zaidi ya Sh. milioni 400 kwa ajili ya kununua vifaa vya redio 16 za kijamii nchini lengo likiwa kuhakikisha jamii inapata habari kwa wakati.

Ni imani yetu kuwa ushirikiano wa vyombo vya habari, serikali na wadau wa habari utaleta mafanikio makubwa katika kuhabarisha umma na kuleta mabadiliko ya kiuchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Beatrice Moses

## Muungwana Lazima Nilonge

### Ibada hizi za mizimu 'kiwazimu' zidhibitiwe

**HIVI** karibuni kuna video iliyozunguka kwenye mitandao kadhaa ya jamii, iliyowaonyesha familia ya watu wanane waliotembea kilometa kadhaa bila mavazi, wakidai wanafanya hivyo kuitii mizimu.

Kutokana na tukio hilo Mkuu wa Wilaya ya Morogoro, Bakari Msulwa, alilazimika kuitembelea familia hiyo iliyotajwa kuwa ni ya Seleman Mpange, mkazi wa Kijiji cha Lukulunge katika Manispaa ya Morogoro, kujua kulikoni.

Watu wanane wa familia hiyo wakiwamo baba, mama na watoto na mkwe kwa pamoja walivua nguo na kutembea umbali wa zaidi ya kilometa tatu asubuhi ya Aprili 7, mwaka huu, wakidaiwa kuwa wanatekeleza masharti ya mizimu ya ukoo huo.

Baba wa familia, Mpange baada ya kuhojiwa na Mkuu wa Wilaya alieleza kuwa ameamua kufanya hivyo ili kutii masuala ya mizimu, mila na desturi za ukoo wao.

Mkuu wa Wilaya alishauri suala hilo kuzungumzwa kifamilia ili kubaini ukweli wa jambo hilo wakiwashirikisha wazee wa kimila.

Kwa upande mwingine uamuzi huu ni mzuri ingawa kulingana na taharuki waliyoisababisha kwenye jamii haitoshi kuchukua maamuzi hayo, hatua zaidi zilihitajika ili kuifunza jamii kuishi maisha yenye maadili.

Masuala ya dini yanayohusishwa na imani za kiroho ni jambo ambalo halipingwi kwani kila mtu ana haki ya kuabudu imani yake, lakini serikali haina dini licha ya kwamba imekuwa ikihusika katika kusimamia masuala ya dini zote.

Lengo la serikali ni kujiridhisha kuwa dini zinaendeshwa katika misingi ambayo havunji amani ya nchi wali haivurugi ustawi wa taifa.

Ni wazi kuwa kila mtu ana uhuru wa kuchagua dini anayoipenda zikiwamo za jadi kutegemea na jinsi imani ya familia yake au maamuzi yake ama alivyovutika na taratibu za kuabudu zinazotumika.

Kitendo walichofaya familia hiyo ni wazi kuwa kilitumia vibaya uhuru uliopo wa kuabudu kulingana na maadili ya nchi hii, pia ilisababisha kuvunja heshima yao na kuweka kumbukumbu mbaya ya watoto wao kwenye jamii kutokana na kutembea utupu.

Tumeshawahi kusikia visa kadhaa kwenye dini mbalimbali duniani, vikiwamo vinavyohusu viongozi wa madhehebu ya dini hizo kushawishi waumini wao kutenda mambo ambayo yanasababisha fedheha, mateso hadi vifo.

Nchini Uganda miaka kadhaa iliyopita kiongozi mmoja wa dini aliyetambulika kwa jina la Kibwetere alisababisha vifo vya waumini wake kwa kuwasha moto akiwaaminisha kuwa ndiyo mwisho wa dunia lakini alitoweka na hakuwa pamoja nao na kusababisha vifo vya maelfu.

Hivyo kuna umuhimu wa kudhibiti dini ama madhehebu mbalimbali hasa wa kuwa mafundisho yanatofautia kulingana na njia za ufundishaji.

Jambo lingine ni kuwa kutokana na sayansi na teknolojia tukio hilo tayari limehifadhiwa hivyo limeweka kumbukumbu mbaya ya kudumu kuhusu familia hiyo, ambayo inaweza kuwagharimu watoto wao ikiwamo hata kuwakosesha amani na fursa mbalimbali.

Kwa mujibu wa andiko lililopo kwenye kitabu cha Falsafa ya Sanaa Tanzania (Baraza la Sanaa la Taifa 1982) inabainishwa kuwa tambiko ni miongoni mwa mambo ambayo yamekuwa yakifanywa na jamii za Tanzania.

Ni ni ibada inayohusisha kuipa mizimu heshima na sadaka ili jamii inayohusika ipate amani, kwa kuzingatia kanuni za ibada hizi hazikuruhusu watu kumwendea Mwenyezi Mungu moja kwa moja hivyo hupitishia maombi yao kwa mizimu, sadaka kwa njia ya tambiko, ni ili ifurahi, itulie, ipate kuyafikisha maombi ya watambikaji kwa Mwenyezi Mungu na kumsihi ayakubali.

Hata hivyo, uhuru wa kuabudu usitumiwe vibaya na kusababisha jamii kupatwa na aibu kwa kujiingiza kwenye mambo ambayo hayana tofauti na yale yanayofanywa na watu wasio na elimu wa maarifa ya kutambua kuwa kutembea bila mavazi ni hatia si mbele ya sheria bali hata kwa jamii inayowazunguka.

# HABARI PICHA




Mabalozi wa Canada na Uingereza wakitembelea chumba cha kutayarisha vipindi cha East Africa Radio na Televisheni. **PICHA ZOTE: SELEMANI MPOCHI**



Mkuu wa Chaneli wa ITV, Pius akiwaeleza mabalozi wa Uingereza na Canada walipotembelea chumba cha kurushia matangazo cha ITV.



Mabalozi wa Uingereza, David Concar (kushoto) na Pamela O'Donell (Canada) wakiwa katika chumba cha kurushia taarifa ya habari cha ITV.



Naibu Mkurugenzi wa Radio One/ Capital Radio, Abdallah Mwaipaya akitoa maelezo jinsi ya kurusha matangazo.



Meneja wa Kiwanda cha Uchapaji Magazeti cha The Guardian Ltd, BalaSubramanian Venkadachalam, akiwaonyesha Balozi wa Uingereza nchini, David Concar na Balozi wa Canada nchini, Pamela O'Donell, jinsi mtambo wa kuchapishia magazeti unavyofanya kazi.

# TIC yahakikishia wakulima soko

**Na Richard Makore,** MWANZA

KITUO cha Uwekezaji (TIC), kimewahakikishia wakulima soko la kuuza bidhaa zao baada ya baadhi ya viwanda kuongeza uzalishaji.

Akizungumza ofisini kwake hivi karibuni jijini Mwanza, Meneja wa TIC Kanda ya Ziwa, Pendo Gondwe, alisema viwanda vingi vimeongeza uzalishaji, na kwamba soko la mazao ya wakulima litaongezeka.

Akizungumzia uwekezaji katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kwa sasa, Pendo alisema wawekezaji wanne wa viwanda vikubwa wametoa ajira 7,820 kwa Watanzania.

Alisema kutokana na mazingira mazuri yaliyowekwa na serikali, viwanda hivyo vimeendelea kufanya uzalishaji, hivyo kuongeza ulipaji wa kodi za serikali.

Aidha, Pendo alisema kiwanda cha kuchakata pamba cha Alliance Ginnery cha mkoani Simiyu kwa mwaka kinachakata tani 30,000 za pamba ambayo kinanunua kutoka kwa wakulima.

Alisema uchakataji huo bado upo chini, na kwamba kuna uwezo wa kuchakata tani 100,000 kama malighafi ya pamba itapatikana.

Alisema viwanda vingine ambavyo TIC Kanda ya Ziwa ilitembelea na kukagua shughuli za uwekezaji ni cha sukari mkoani Kagera.

Katika kiwanda hicho, Pendo alisema ifikapo mwaka 2030 kitakuwa na uwezo wa kuzalisha sukari tani 250,000, ambayo itauzwa ndani ya nchi, hivyo kuokoa dola za Marekani milioni 100 ambazo zinatumiwa na serikali kuagiza bidhaa hiyo kila mwaka.

Akizungumzia kiwanda cha Jambo Food Products cha mkoani Shinyanga, alisema kinachakata matunda mbalimbali ambayo yanatoka kwa wakulima.

Hatua hiyo inawawezesha wakulima katika mikoa ya Kanda ya Ziwa kupata fursa ya kuuza matunda yao pamoja na asali katika kiwanda hicho.

Kwa upande wa kiwanda cha kahawa cha Amir Hamza kilichopo mkoani Kagera, meneja huyo wa TIC Kanda ya Ziwa alisema kwa sasa kina uwezo wa kununua asilimia 50 ya bidhaa.

Alisema wakulima wa zao hilo katika mikoa mbalimbali kwa sasa wana uhakika wa soko, na kwamba kinachakata tani 300 za kahawa kwa mwaka.




Kaimu Mkurugenzi wa Bank of Africa, Wasia Mushi (kushoto), akimkabidhi Meneja Mipango wa Taasisi ya Kalamu Education Foundation, Said Ali, sehemu ya msaada wa vyakula mbalimbali kwa ajili ya futari kwa watoto yatima, wajane na wazee. Msaada huo ulikabidhiwa Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Barrick kinara usalama na afya mahali pa kazi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya uchimbaji madini ya Barrick Gold Corporation imeshika nafasi ya kwanza katika Tuzo za Usalama na Afya Mahala pa Kazi kwa mwaka huu kwa upande wa Sekta ya Madini.

Tuzo hiyo inayotolewa na Mamlaka ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA), ilikabidhiwa wakati wa maadhimisho ya kilele cha Siku ya Usalama na Afya Mahala pa Kazi Duniani ambayo kitaifa ilifanyika jijini Mwanza.

Taarifa iliyotolewa na uongozi wa Barrick jana, ilibainisha kuwa ushindi wa tuzo hiyo iliyokabidhiwa kwa kampuni na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, ni matokeo ya juhudi za makusudi ambazo kampuni imekuwa ikizitekeleza katika kulinda, kuhamasisha na kuimarisha usalama na afya kwa wafanyakazi wake, makandarasi na wadau mbalimbali inaoshirikiana nao.

"Kampuni inawashukuru wafanyakazi wake, makandarasi na wadau wote kwa kuunga mkono sera, mikakati na miongozo yake inayolenga kuhimizana na kukumbushana umuhimu wa kuzingatia bila shuruti usalama na afya ya kila mmoja wakati anapotimiza majukumu yake, bila hivyo mafanikio haya ya ushindi yasingepatikana," Barrick ilibainisha katika taarifa hiyo.

Kampuni hiyo ilibainisha kuwa imejiwekea lengo la kuhakikisha kanuni za usalama zinatekelezwa ipasavyo katika maeneo yake yote ya kazi kufikia viwango vya kimataifa.

# Walimu wakuu washindwa wimbo wa Afrika Mashariki

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WALIMU wakuu katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wameshindwa kuimba wimbo wa Afrika Mashariki mbele ya Mkuu wa wilaya hiyo, Anamringi Macha, wakati wa ufunguzi mafunzo ya kuwajengea uwezo juu ya kutambua mambo mbalimbali yanayohusu skauti.

Walimu hao ni wa shule za msingi, sekondari na maofisa elimu kata licha ya Mkuu wa Wilaya kutoa Sh. 50,000 kwa atakayeweza kuimba, lakini walishindwa.

Macha aliwataka walimu hao kuimba wimbo wa Afrika Mashariki wakati akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kutambua mambo mbalimbali yanayohusu skauti.

Alisema wimbo huo ni sehemu ya Wimbo wa Taifa wa Tanzania, lakini anashangaa kuona walimu hawajui kuimba.

"Ninatoa kiasi cha Sh. 50,000 kwa mshiriki yeyote katika ukumbi huu kujitokeza mbele na kuimba wimbo wa Afrika Mashariki walau kuimba hata beti mmoja nitampa kiasi hiki," alisema Macha.

Macha aliwataka viongozi wa skauti kuhakikisha wanafundisha walimu na wanafunzi shuleni wimbo huo, na kama kutakuwa na gharama zozote kwa ajili ya uchapishaji yeye yupo tayari kugharamia ili kila mwanafunzi apate nakala ya wimbo.

Alisema kuwa wananchi wengi hapa nchini hawajui kuimba wimbo huo huku akiwataka waandaaji wa semina hiyo ambao ni skauti kutomualika tena katika ufunguzi huo kama wimbo huo hautakuwa ukipigwa katika mafunzo yao.

Kwa upande wake Kamishna wa skauti wa Mkoa wa Shinyanga, Mussa Chama, aliwataka walimu kuhakikisha wanawatumia skauti katika ulinzi mdogo shuleni kabla ya masomo na nyakati za mapumziko ili kuwawekea ari ya uzalendo ya kulinda nchi yao.

# HABARI KITAIFA

## Kampuni ya bima AAR yaja kivingine

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bima AAR imezindua rasmi jina jipya la kampuni, Assemble Insurance Company Limited.

Mwakilishi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima (TIRA), Saidi Mpombo ambaye alikuwa mgeni rasmi katika hafla hiyo, wakati wa iftari jijini Dar es Salaam, aliipongeza kampuni hiyo kwa hatua ya kufanya umiliki wa kamapuni hiyo kuwa wa kitanzania kwa asilimia 100.

Mpombo alisema anaamini tukio hilo la kihistoria la kampuni hiyo litaenda sambamba na uboreshaji wa huduma za bima zilizokuwa zinatolewa pamoja na upanuzi wa kampuni hiyo.

"Kwa dhati, niwapongeze kampuni ya Assemble kwa hatua walioifikia, hususan kwa kufanya umiliki wa kampuni hii kuwa wa kitanzania kwa asilimia 100. Hatua ambayo itahamasisha ushiriki wa Watanzania katika kuwekeza kwenye sekta hii ya bima nchini, hivyo kuongeza wawekezaji wa ndani," alisema Mpombo.

Aliongeza kuwa mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya serikali itaendelea kusimamia sheria kwa dhati, hivyo kuwawekea mazingira mazuri wawekezaji wa ndani na wa nje kuwekeza kwenye sekta ya bima nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Assemble Insurance Company Limited (zamani AAR), Violet Mordichai, alisema mabadiliko hayo ni sehemu ya mchakato wa ujengaji na uboreshaji wa kampuni hiyo.

Alisema, kabla ya kubadilisha jina, kampuni hiyo ya bima ilifanikiwa kufanya mabadiliko makubwa ya kubadili kabisa mfumo wake wa hisa kuwa katika ngazi ya Tanzania kwa asilimia 100 na kutenganisha kuwa taasisi tofauti.

"Hapo awali AAR ilikuwa inajulikana kwa utoaji wa bima ya afya, lakini kwa sasa kama jina jipya la Kampuni, Assemble Company Limited, tutakuwa tukitoa huduma mbalimbali za bima chini ya mwamvuli mmoja. Jina jipya lenyewe linaonyesha ukusanyaji wa huduma, wa bima zote kwa ujumla ikiwamo na za afya," alisema Modichai.

Pia aliahidi kuwa kampuni itaendelea kutoa huduma za kipekee kwa wateja wao, kwa kutoa suluhisho la bima na la kiushindani.

Alisema kwa wale watakaochagua huduma ya bima ya afya, na mathalani bima yao inatoa fidia wapatapo majeraha ya mwili yanayosababishwa na vurugu, ajali au njia mbalimabli zinazoonekana.

Huduma hiyo ya bima kwa mujibu wa Mordichai inapatikana kwa watu binafsi na familia, wafanyabiashara wadogo pamoja na kampuni.

# Mil.178/- kumtua ndoo kichwani mwanamke

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKALA wa Maji Vijijini (RUWASA) wilayani Shinyanga mkoani hapa, umetumia Sh. milioni 177.9 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa majisafi na salama katika Kijiji cha Ihapa Manispaa ya Shinyanga na kumtua ndoo kichwani mwanamke.

Meneja wa RUWASA wilayani Shinyanga, Emael Nkopi, alibainisha hayo juzi, wakati akisoma taarifa kwenye uzinduzi wa mradi huo wa majisafi na salama katika kijiji hicho kutoka Ziwa Victoria, uliozinduliwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Jasinta Mboneko.

Alisema mradi huo ulianza kutekelezwa Novemba mwaka jana, na ulikamilika mwezi uliopita na utahudumia wananchi 3,535 katika kijiji hicho na kwamba umegharimu Sh. milioni 177.9. na kumtua ndoo kichwani mwanamke.

"Manufaa ya mradi huu ni kuwaondolea wananchi kero ya kutafuta majisafi na salama umbali mrefu, na kuokoa muda wa kufanya shughuli zao za uzalishaji mali na kuinuka kiuchumi," alisema Nkopi.

Naye DC Mboneko, aliwataka wananchi kuitunza miundombinu ya mradi huo pamoja na kuepuka 'vishoka' kuwatapeli fedha, wakiwarubuni watawaunganishia maji majumbani mwao, bali shughuli hiyo itafanywa na mamlaka za maji.

Mmoja wa kinamama katika kijiji hicho, Zena Ibrahimu, alisema mradi huo ni mkombozi kwao, ambapo pia utaleta amani katika ndoa zao.




Mkurugenzi Mkuu wa Assemble Insurance Limited, Violet Mordichai pamoja na Bodi ya Wakurugenzi ya kampuni hiyo wakizindua rasmi nembo mpya ya kampuni ya Assemble Insurance Limited (iliyokuwa ikijulikana AAR Insurance). Kushoto kwake ni mwakilishi wa TIRA, Said Mpombo, jijini Dar es Salaam. **PiCHA: MPIGAPICHA WETU**

# WLAC yajikita 'kunoa' wafanyakazi kudai haki

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Msaada wa Kisheria kwa Wanawake (WLAC), kimesema bado juhudi kubwa inahitajika katika kuelimisha wafanyakazi namna ya kudai haki zao kazini pale zinapokiukwa.

Akizungumza wakati akitoa elimu kwa wafanyakazi katika sekta isiyo rasmi katika Kata ya Tandika wakiwamo mamalishe, wafanyakazi wa majumbani, hotelini na wengine katika sekta isiyo rasmi, Ofisa Sheria kutoka WLAC, Barcoal Deogratius, alisema wamebaini kwamba bado baadhi ya wafanyakazi hawajatambua haki zao kazini.

Deogratius alisema katika shughuli mbalimbali za kuelimisha wafanyakazi wanazotoa katika sekta rasmi na isiyo rasmi, wamekuwa wakikumbana na baadhi ya wafanyakazi hususani katika sekta isiyo rasmi wakiwa wamekata tamaa ya kufuatilia haki zao za msingi baada ya kuondolewa kwenye ajira na waajiri wao.

"Katika kutoa semina kwa nyakati tofauti, WLAC tumekuwa tukikumbana na kesi tofauti kutoka kwa wafanyakazi, hasa wale ambao wamekatishwa ajira zao, na wengi wao baada ya kukumbwa na tatizo hilo hukata tamaa na kushindwa kupigania ili wapate haki zao za msingi," alisema Deogratius.

"Baadhi yao wananyimwa kupewa stahiki zao au wengine wananyimwa mikataba, wanafukuzwa kazi kiholela, wananyimwa likizo, kunyanyaswa kingono na kunyimwa malipo ya kazi za ziada, lakini hawajui waanzie wapi kudai haki na ndiyo maana tukaamua kuja na mradi wa kutoa elimu hii na tunashukuru kwa sasa umeanza kuwasaidia."

Alisema ni vema kila mfanyakazi bila kujali sekta aliyopo kuhakikisha kwamba anafahamu haki zake za msingi awapo kazini.

"Wafanyakazi wote mahali walipo wanatakiwa kufahamu haki zao, haijalishi wako katika sekta rasmi au isiyo rasmi, kila mtu anapofanya kazi mahali popote ana hitaji kupata haki zake za msingi kwa sababu sheria inayoongoza haki za wafanyakazi iko moja tu ambayo ni ya mwaka 2004," akisema na kuongeza:

"Na hiyo ndio inayosimamia masuala yote ya kazi iwe sekta rasmi au isiyo rasmi, kwa hiyo wafanyakazi wanatakiwa walitambue hilo bila kujisikia wanyonge."

Kwa upande wake, Rodgers Michael, Ofisa Sheria WLAC, alisema imefika wakati sasa ambapo kila mfanyakazi hatakiwi kukubali kunyanyasika kwa namna yoyote kwa sababu ya kunyimwa haki zake za msingi zinazohusu ajira.

"Ndio maana sisi wanasheria tupo hapa, WLAC sisi tumekuwa tukipokea kesi kwenye eneo hili na tumewasaidia wengi, kwa ushauri wangu ni kwamba unapopata manyanyaso ambayo unahisi kabisa ni kinyume cha sheria usisite kutuona ili tukushauri namna ya kufanya," alisema Michael.

# Mamilioni yatengwa daraja la Mto Bubu

SERIKALI imesema katika mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22, imetenga Sh. milioni 66 kwa ajili ya kukamilisha kazi ya usanifu wa daraja jipya katika Mto Bubu lililoko Kondoa Mjini mkoani Dodoma.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, alibainisha hayo jana bungeni alipojibu swali la Mbunge wa Kondoa Mjini (CCM), Ali Makoa.


Mbunge huyo alihoji ni lini serikali itaanza kujenga daraja hilo ili wananchi wa upande wa pili wa mto wavuke na kupata huduma mbalimbali za kijamii.

Akijibu swali hilo, Waitara alisema taratibu za ununuzi wa kumpata mhandisi mshauri zipo katika hatua za mwisho na kazi hiyo inatarajiwa kuanza mwezi ujao.

Alisema daraja hilo lijulikanalo kama Munguri B lipo katika barabara ya Kondoa – Nunguri– Mtiriangwi – Gisambalang – Nangwa yenye jumla ya urefu wa kilometa 81.4.

"Barabara hii inaunganisha Mkoa wa Dodoma na Manyara kupitia Wilaya za Kondoa na Hanang kutokana na mvua kubwa zilizonyesha mwaka 2019/2020 zilisababisha Mto Bubu kutanuka na kufanya Daraja la Munguri B kutopitika wakati wa mvua," alisema.

Naibu waziri huyo alisema kuwa baada ya usanifu kukamilika, ujenzi wa daraja hilo utaanza kulingana na upatikanaji wa fedha.



Habari zote na Augusta Njoji

# Waziri apiga 'stop' shule kudai cheti cha awali

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amepiga marufuku shule kudai cheti cha elimu ya awali kwa wanafunzi wanaoanza darasa la kwanza.

Ummy alitoa kauli hiyo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mariam Kisangi.

Mbunge huyo alitaka serikali itoe tamko kuhusu sharti la kuwa na cheti cha elimu ya awali ndipo mtoto ajiunge na darasa la kwanza.

Pia alihoji mpango wa serikali kuweka bajeti ya kutosha ya elimu ya awali katika shule zote za msingi.

Ummy, akitoa tamko la serikali, alisema ni marufuku kwa shule kudai cheti hicho na kuahidi wabunge kuwa serikali itahakikisha watoto wanapata elimu bila kikwazo.

"Wale wanaodai cheti watambue wanaenda kinyume cha miongozo na taratibu za serikali," alisema.

Awali, Naibu Waziri David Silinde alisema serikali haina utaratibu wa kutoa cheti cha elimu ya awali na kwamba utaratibu huo wa kujitungia unafanywa na shule binafsi.

"Huo utaratibu haupo na 'certificate' (cheti) za serikali za darasa la saba, kidato cha nne, sita na kuendelea, shule za awali 'certificate' hamna na ni utaratibu ambao serikali haiutambui," alisema.

Katika swali la msingi la mbunge huyo, alisema utaratibu wa watoto kuingia darasa la kwanza ni lazima awe amepitia shule za awali.

"Je, serikali ina mpango gani wa kuimarisha madarasa ya elimu ya awali?" Mbunge huyo alihoji.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema elimu ya awali ni muhimu katika kumwandaa na kumjengea msingi mwanafunzi wakati wote atakapokuwa anaendelea na masomo katika ngazi zote.

"Kwa kuzingatia suala hili, serikali ilitoa maagizo kuwa kila shule ya msingi nchini iwe na darasa la awali ili kuwapokea wanafunzi walio na umri wa miaka mitano hadi mitano ikiwa ni maandalizi ya kujiunga na darasa la kwanza," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali imeandaa mtaala wa elimu ya awali unaoendana na aina ya ujifunzaji unaotakiwa kwa watoto wa elimu ya awali na mtaala huo umezingatia ujifunzaji kwa kutumia michezo.

"Hadi Februari 2021, walimu 70,712 wanaofundisha darasa la awali, la kwanza na la pili wamepatiwa mafunzo ya namna ya utumiaji wa mbinu sahihi za ufundishaji, ufaraguzi na utumiaji wa zana za kufundishia, hatua hii imeimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika madarasa ya awali nchini," alisema.

Alisisitiza serikali itaendelea kuboresha miundombinu na kuwajengea uwezo walimu wanaofundisha elimu ya awali katika shule zote nchini kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge, Kazi, Ajira,Vijana na Walemavu, Jenista Mhagama, akikabidhi kikombe kwa Meneja Usalama wa mgodi wa Barrick wa Bulyangulu, Dk. Kudra Said Mfaume, Barrick Tanzania baada ya kuibuka mshindi wa kwanza katika kundi la migodi. Hafla ya kukabidhi tuzo ilifanyika wakati wa kilele cha maonyesho ya Wiki ya Afya na Usalama Mahali pa Kazi yaliyoandaliwa na OSHA jijini Mwanza. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Serikali yaanika mkakati kudhibiti matumizi zebaki

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa ndani ya miezi miwili uagizaji wa kemikali ya zebaki utakuwa umedhibitiwa na kutakuwa na chanzo kinachoeleweka.

Waziri wa Madini, Dotto Biteko, aliyasema hayo bungeni jana alipojibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Kabula Shitobelo.

Mbunge huyo alisema Kanda ya Ziwa kuna tatizo kubwa la saratani na anaamini zebaki ndiyo inayosababisha ongezeko la tatizo hilo.

"Serikali ina mpango gani wa kudhibiti uingizaji wa kemikali ya zebaki ili kunusuru wananchi wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Biteko alisema Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Wadogo (FEMATA) kwa kushirikiana na Mkemia Mkuu wa Serikali, wanatengeneza mwamvuli mmoja wa kuagiza kemikali ya zebaki nchini.

"Mkemia Mkuu wa Serikali ameshatoa hiyo 'go ahead' (kuendelea na mchakato), changamoto tuliyonayo ilikuwa ni ndogo ndogo ya uratibu," alisema.

Waziri huyo alisema mialo ya uchenjuaji wa madini ipo 5,025 na imesajiliwa nchini ikiwa ni hatua ya serikali ya kudhibiti mialo isiwe holela.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Hawa Mchafu, alihoji ni kwa kiasi gani serikali inafahamu madhara yatokanayo na zebaki.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri wa Madini, Prof. Shukrani Manya, alisema kemikali hiyo inatambua madhara makubwa ya kiafya kwa binadamu, mimea na mazingira yanayosababishwa na matumizi ya kemikali ya zebaki katika shughuli za uchenjuaji madini.

"Miongoni mwa madhara ya kemikali hiyo kwa binadamu ni kuathiri mifumo ya fahamu, uzazi, upumuaji na kusababisha magonjwa mbalimbali kama magonjwa ya figo, moyo na saratani," alisema.

Alisema kemikali hiyo pia huathiri viumbe hai vya majini na nchi kavu pindi zebaki inapotiririka na kuingia kwenye vyanzo vya maji ambavyo hutumiwa kwa matumizi mbalimbali ikiwa ni pamoja na shughuli za kibinadamu.

"Njia zinazopelekea kemikali ya zebaki kuingia mwilini ni kushika, kuvuta hewa na kula vyakula vyenye viambata vya kemikali hiyo," alifafanua.

Alisema kuwa mbali na athari hizo za kiafya, matumizi ya zebaki katika uchenjuaji wa dhahabu pia yameonyesha uwezo mdogo wa kutoa dhahabu ambao ni chini ya asilimia 30 hali ambayo imekuwa ikipelekewa wachimbaji wadogo kushindwa kuzalisha kiwango cha kutosha na hivyo kupata faida ndogo.

"Ili kukabiliana na changamoto hiyo, serikali imekuwa ikitoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu athari za kemikali hiyo na njia salama za utumiaji ikiwa ni pamoja na usakafiaji wa mialo na utumiaji wa retorts (vigida) wakati wa uchomaji.

"Serikali kupitia STAMICO itaendelea kutoa elimu ya matumizi ya njia mbadala ya uchenjuaji dhahabu kwa vitendo kupitia vituo vya mfano vya Lwamgasa, Katente na Itumbi," alisema.

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# Fahamu ilikuwaje jiwe Bismarck kuwa kitambulisho Jiji la Mwanza

UTAMBULISHO wa Jiji la Mwanza kwa wageni na wenyeji ni jiwe la Bismarck, lililopo ndani ya Ziwa Victoria eneo la bustani ya Kamanga Feri.

Mwamba huo ulipewa jina la Mjerumani kwa vile inadaiwa alikuwa mtu wa kwanza (mgeni, Mzungu) kuliona jabali hilo na kulishangaa, huyu alikuwa Otto Von Bismarck, ambaye baadaye alikuwa Kansela wa Ujerumani.

Baada ya kuondoka Mwanza jiwe hilo lililochomoza juu ya maji ya Ziwa Victoria, lilipewa jina lake. Yote hayo yalitokea wakati wa utawala wa Kijerumani takribani miaka 137 iliyopita.

Akizungumza na Nipashe, wakati alipotembelea Mwanza baharia Thomas James, anasema maajabu ya jiwe hili ni pamoja na kuzungukwa na maji, lakini ndani kuna pango lenye ukubwa kama chumba cha kuishi.

Maajabu yanazidi kwa kuangalia namna lilivyokaa ni la kipekee kutokana na jinsi mawe yalivyobebana yanaonekana kama vile yatadondoka, lakini kwa karne nyingi hayajatikisika.

Anasema jiwe la Bismarck ni kati ya chanzo cha mapato kwa mkoa huo. Fedha zinazokusanywa zinatoka kwa watalii wa ndani na nje wanaolizuru eneo hilo huku Ziwa Victoria lililo mama wa jiwe hilo likizalisha kitoweo mujarabu cha samaki wakiwamo sangara, sato na dagaa.

Historia ya jiwe na jina au mwamba huu uliopo ndani ya ziwa hili, liliopo jirani na bustani ya Kamanga Feri ni eneo ambalo hufikiwa na wageni kutoka jijini humo lakini hasa mikoa tofauti achilia mbali watalii kutoka mataifa tofauti.



Jiwe la Bismarck linaloelea kwenye maji ya Ziwa Victoria ni kivutio kikubwa katika Jiji la Mwanza. **PICHA: MTANDAO**

### JIWE LENYEWE

Mwamba huo unaelezewa kwa namna mbalimbali na wakazi wanaoishi jirani na ufukwe wa Ziwa Victoria ambalo ni ziwa kubwa barani Afrika na chanzo cha Mto Nile.

Baharia Thomas James, anayeishi jirani na mwalo anasema: "Ni sehemu ambayo inavutia wageni wanaofika Mwanza. Zaidi tunapokea watalii kutoka nchi tofauti kama Ujerumani na Uingereza. Ninawaongoza nawatembeza katika jiwe hili na maeneo jirani kwa kutumia boti."

Baharia huyo, ambaye ana uzoefu wa takribani miaka 20 katika kufanya shughuli hiyo Ziwa Victoria anasema jiwe hilo awali lilikuwa makazi ya aliyekuwa mtemi wa Wasukuma miaka takribani 100 iliyopita, aliyeitwa Mwanamalundi, ambaye aliongeza zaidi umaarufu wa jiwe hilo.

Kuhusu wanaotembelea eneo hilo, kiimani James anasema, jiwe la Bismarck ni sehemu ya utamaduni wa wenyeji na wengi hufika kutambika kulingana na kile wanachoamini.

"Chifu Mwanamalundi katika jiwe hili aliishi baada ya wakoloni kumtafuta akikimbilia kujificha hapa, ameacha alama za nyayo zake juu ya jiwe hili. Ndani ya pango hili alifanya malazi, kuna jiwe kama kitanda kwa ndani, ambako maji hayaingii hata siku moja wala mvua haifiki," anasema baharia James.

Anaeleza kuwa kutokana na uelewa mdogo kuhusu kuhifadhi maeneo ya kihistoria baadhi ya wakazi hufika eneo hilo wanakwangua sehemu ya unyayo na kwenda kufanyia shughuli mbalimbali zikiwapo ibada na matambiko.

"Pale juu ya jiwe kuna mikuki ambayo aliichomeka siku nyingi. Tumeikuta na tunaamini hivyo, inabidi tupatunze kwa ajili ya utalii kwa kuwa inatuingizia kipato na kuupa umaarufu mkoa wa Mwanza," anabainisha mwongoza watalii huyo.

### FURSA YA AJIRA

Kuhusu namna jiwe hilo kuwa sehemu ya utalii na chanzo cha mapato, anasema ili kufika eneo lililopo jiwe la Bismarck, watalii hulipia fedha ili kufikishwa hapo.

Anabainisha kwamba kabla ya kupanda boti ya kukodi, watalii hutoa kiingilio cha Sh. 1,000 kuingia kwenye geti la bustani ya Kamanga ambayo inasimamiwa na Halmashauri ya Mwanza.

Kadhalika anasema fedha hizo ni maalumu kwa ajili ya kutunza bustani, iliyopo chini ya halmashauri ya manispaa hiyo na kwamba mtunza bustani ana jukumu la kuweka mazingira ya eneo hilo katika hali ya usafi kila wakati.

Anasema kwa watalii ambao wanahitaji kutembezwa maeneo tofauti yaliyo jirani na jiwe hilo, wanatozwa Dola 100 au Shilingi 230,000 kwa saa moja mpaka saa 1.30, kwa kutumia usafiri wa boti ya kukodi kulifikia jiwe la Bismarck lililo umbali wa takribani mita 200 kutoka bustani hiyo.

"Wageni wa ndani ya nchi wanalipia Sh. 10,000 kwa mtu mmoja kwenda kutembezwa na boti kwenye maeneo tofauti yaliyo jirani na jiwe la Bismarck," anaeleza, James.

Jessica Masanja ambaye anafanya shughuli za kuuza samaki sokoni anasema eneo hilo ni makumbusho ambayo yanahitaji kuhifadhiwa.

Anasema historia ambayo ameikuta na kupata simulizi ndani ya jiwe hilo inasemekana mtemi Mwanamalundi aliishi miaka mingi na kupata huduma za kibinadamu za kila siku ikiwamo kujipikia ndani ya pango hilo.

> "Wageni wa ndani ya nchi wanalipia Sh. 10,000 kwa mtu mmoja kwenda kutembezwa na boti kwenye maeneo tofauti yaliyo jirani na jiwe la Bismarck.

### HISTORIA JINA BISMARCK

Kansela Otto von Bismarck, kwa mujibu wa mtandao alizaliwa Aprili 1, 1815 na kufariki Julai 30, 1898 na kwamba alikuwa mwanasiasa mashuhuri wa Ujerumani katika karne ya 19 na kuwa Waziri Mkuu wa Prussia.

Inaelezwa kuwa alijenga Umoja wa Wajerumani katika vita tatu dhidi ya Denmark ya mwaka 1864, Austria 1866 na Ufaransa iliyoanza 1870 hadi 71.

Kama Kansela wa Dola la Ujerumani aliongoza siasa ya nchi hadi 1890 alipoondolewa ikulu na Kaisari kijana Wilhelm wa II.

### MTEMI WA WASUKUMA

Mwanamalundi alikuwa mcheza ngoma mashuhuri kutoka kabila la Wasukuma ambaye alipewa jina hilo kama utani likimaanisha miguu myembamba na mirefu, alizaliwa katika Kijiji cha Mwakubunga Nera katika Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza mwaka 1846.

Umahiri wake wa kucheza ngoma mara nyingi alifuatwa na kundi la watoto kwa sababu ili kumshuhudia. Wazazi wake hawakufurahia hilo, kutokana na kwamba watoto ambao waliwategemea katika kupeleka mifugo machungani, waliitelekeza mifugo na kumfuata Mwanamalundi na kusababisha kupotea kwa watoto na mifugo yao.

# Tamko la HakiElimu Juu ya Upangaji wa Bajeti ya Sekta ya Elimu kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 Tarehe 3 Mei 2021

**1. Utangulizi**

Tunatambua Serikali ya Jamhuli ya Muungano ya Awamu ya Tano ilitilia mkazo na kuweka mipango mbali mbali iliyolenga kupanua fursa za kupata elimu ya msingi na sekondari hasa kwa watoto wa familia zenye kipato cha chini. Baadhi ya mipango hiyo ni pamoja na utoaji wa Elimumsingi bila ada, ambao umesaidia kutoa fursa kwa watoto wengi kudahiliwa kwenye shule za msingi na sekondari. Kwa elimu ya msingi, idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka mil 8.2 mwaka 2016 hadi mil 10 mwaka 2020. Hivyo inatarajiwa wanafunzi wengi kuongezeka kwenye shule za sekondari kutoka mil 2.6 mwaka 2020 hadi wanafunzi mil 4.5 kufikia mwaka 2024(BEST 2020). Hii ni kwa sababu wanafunzi wengi waliodahiliwa kwenye shule za msingi kuanzia mwaka 2016 wataanza kumaliza elimu ya msingi mwaka 2021 na hivyo watahamia shule za sekondari miaka minne ijayo.

Kwa kutambua umuhimu wa mipango na malengo hayo katika elimu, na kwa kuzingatia kuwa vikao vya Bunge la Bvya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Mama Samia Suluhu Hasan vimeanza, HakiElimu tumeona ni busara kutumia wasaa huu kukumbushana sehemu ya hiyo mipango ambayo inahitaji uwekezaji wa kibajeti.

Tamko hili, linawasilisha sehemu ya hiyo mipango na azma za kielimu ambazo zilikwisha anza kujadiliwa na kufanyiwa kazi. Nia yetu ni kuona mipango hii inajadiliwa Bungeni, inapewa kipaumbele na kutengewa Bajeti na mpango mkakati wa utekelezaji wake katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kuendelea.

**2. Azma ya utoaji Elimu bila Ada**

Kupitia Waraka wa Elimu Namba 5 wa Mwaka 2015 na Namba 3 wa Mwaka 2016, pamoja na nyaraka nyingine zilizoambatana na hizo; Serikali ya Awamu ya Tano iliazimia na kuanza kutekeleza utoaji wa Elimumsingi bila malipo. Azma hii ilitokana na Mpango utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 iliyolenga kuhakikksha kila mtoto anapata elimu ya msingi na sekondari bila vikwazo – vikiwamo vya kifedha.

Kwa mujibu wa Waraka Namba 3 wa Mwaka 2016, chini ya Mpango wa Elimu Bila Malipo, mwanafunzi atasoma 'Elimumsingi' bila yeye, mzazi au mlezi wake kulipa ada na michango yote iliyokuwa ikitozwa kabla ya Waraka Namba 5 wa Mwaka 2015 kutolewa.

Kabla ya Waraka Namba 5 wa Mwaka 2015; Waraka wa Elimu Namba 11 wa Mwaka 2004 uliwataka wanafunzi wa kutwa kulipa ada ya TShs. 20,000 kwa mwaka, kila mmoja na TShs. 40,000 kwa mwaka, kwa wanafunzi wa bweni. Wanafunzi pia walipaswa kulipia ada ya mitihani kupitia Waraka Namba 1 wa Mwaka 2012, gharama za ukaguzi kupitia Waraka Namba 1 wa Mwaka 2013 na michango mingine kadri Bodi za Shule zilivyoshauri na kukubaliana kupitia Waraka Namba 8 wa Mwaka 2011.

Pamoja na ada na michango hiyo; Serikali bado ilihusika moja kwa moja kupeleka fedha mashuleni kupita ruzuku ya Tshs. 10,000 kwa kila mwanafunzi kwa shule za msingi na TShs. 25,000 kwa kila mwanafunzi kwa shule za sekondari. Hiyo ilifanya Serikali kutenga kwa wastani zaidi ya TShs. bilioni 298 kila mwaka (Citizen Budget 2020/21), sawa na wastani wa TShs billion 24.8 kila mwezi, kuwezesha upatikanaji wa Elimumsingi bila malipo.

Pamoja na juhudi hizi, zilikwepo na chagamoto kadhaa za utekelezaji wa utoaji elimu bila ada ambazo ni muhimu kuziangalia kibajeti. Changamoto hizo ni kama zifuatazo:

**Changamoto za Kiwango cha Ruzuku kuwa Kidogo.**

Ni wazi kuwa kiwango kinachotolewa kama ruzuku shuleni hakitoshi. Hii inathibitishwa na hali halisi iliyoko mashuleni hasa kwa kuangalia gharama za mitihani, uhaba wa vifaa vya kufundishia na michezo, ukosefu wa fedha za utawala n.k. Kwa mujibu wa miongozo, asilimia 40 ya ruzuku shule za msingi na asilimia 50 ya shule za sekondari hubakia Serikalini kwa ajili ya kununua vitabu. Kwa hivyo ni Tshs. 6,000 tu kwa mwanafunzi wa shule ya msingi na TShs. 12,500 tu kwa shule ya sekondari, hufika shuleni kwa ajili ya kugharamia mahitaji ya kumweka mwanafunzi shuleni kama shughuli za utawala, michezo, mitihani, ukarabati na malipo ya wafanyakazi wasio walimu kama walinzi au walimu wa kujitolea. Fedha hizi ni kidogo sana kuendesha shule hasa kwa shule zenye wanafunzi kati ya 300 hadi 400 ambapo kwa shule za msingi zinapata wastani wa TShs 150,000-200,000 kwa mwezi. Ni vigumu kuendesha shule kukidhi gharama za kuchapisha mitihani ya mihula, gharama za vifaa kama chaki, na ukarabati, pamoja na garama za utawala kwa kiasi hiki kwa mwezi

Pia ikumbukwe kuwa mpango wa awali wa utoaji ruzuku mashuleni chini ya MMEM na MMES; ilipendekezwa kiwango cha Dola 10 za Kimarekani kwa kila mtoto (Kwa thamani ya sasa ni takribani Tshs 23,000) kwa shule za msingi na Dola 25 za Kimarekani (Takribani TShs. 55,000 kwa sasa) kwa shule za sekondari.

Ni wito wetu kwa Seikali na Wabunge kuanza mjadala wa upangaji wa fedha za ruzuku kwa kuzingatia mipango ya awali ya MMEM na MMES ambayo imeainisha vizuri mahitaji kwa kuzingatia mabadiliko ya thamani ya fedha na gharama za maisha. Ni pendekezo letu, Bajeti hii na Bajeti zijazo zipandishe na zianze kutenga kiwango cha ruzuku cha TShs. 25,000 kwa kila mwanafunzi wa shule za msingi na TShs. 50,000 kwa shule za sekondari.

**Fidia ya Ada kwa Shule za Sekondari**

Katika utekelezaji wa utoaji elimu bila malipo, Serikali inawajibika kufidia ada ya masomo ambayo wanafunzi wa sekondari walikuwa wakilipa kupitia Waraka wa Elimu Namba 11 wa Mwaka 2004, uliowataka wanafunzi wa

## TANGAZO

kutwa kulipa ada ya TShs. 20,000 kila mmoja na TShs 40,000 kwa wanafunzi wa bweni. Ikumbukwe kabla ya Waraka Namba 11 wa Mwaka 2004, Waraka wa Elimu Namba 9 wa Mwaka 1998 ulielekeza tozo ya ada kuwa TShs 40,000 kwa wanafunzi wa sekondari wa kutwa na TShs. 70,000 kwa wanafunzi wa bweni.

Ni wito wetu kuwa, kutokana na changamoto zilizoko mashuleni, na kutokana na kuongezeka kwa gharama za maisha na mahitaji, Serikali irejee katika viwango vya fidia ya ada kama vilivyoelekezwa katika Waraka Namba 9 wa Mwaka 1998 ambavyo vitazifanya shule za sekondari kupata fidia ya ada ya TShs. 40,000 kwa kila mwanafunzi wa kutwa na TShs. 70,000 kwa kila mwanafunzi wa bweni. Hii itaongeza kiwango cha fedha zinazokwenda moja kwa moja shuleni kusaidia uendeshaji wa shule ambazo kwa mujibu wa ripoti mbalimbali zinakutwa na changamoto nyingi.

**Ruzuku kwa Makundi Maalumu na Elimu Jumuishi**

Waraka Namba 3 wa Mwaka 2016 unatoa maagizo kwa wakurugenzi wa wilaya, miji, manipsaa na majiji; kutenga fedha ya ruzuku ya uendeshaji wa shule kwa asilimia 60 kwa shule za msingi na asilimia 50 kwa shule za sekondari, kwa ajili ya kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa elimu maalumu.

Hapa kuna maswali muhimu ya kujiuliza; na ni Rai yetu kwa wabunge kuiuliza Serikali na kupata majibu. "Fedha hizi za ruzuku kwa ajili ya elimu maalumu ni zipi?" Ni sehemu ya ile ruzuku inayotolewa kwa watoto wote au hii ni tofauti? Ikiwa ni tofauti, tunaomba Serikali ifafanue ruzuku hii hutolewa wakati gani na ni kiasi gani? Tafiti na taarifa za upokeaji fedha mashuleni hazionyeshi kama kuna ruzuku ya aina mbili ambayo huzifikia shule zaidi ya zile TShs 6,000 kwa shule za msingi na TShs 12,500 kwa shule za sekondari, kwa kila mwanafunzi.

**Changamoto ya Kikokotoo Kipya cha Ruzuku**

Kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Sera ya 'Elimu Bila Malipo', HakiElimu tumeonyesha na kuendelea kuishauri Serikali juu ya mapungufu ya kanuni au kikokotoo cha upangaji na ugawaji wa fedha za ruzuku. Kikokotoo kinachotumika sasa hakizingatii utofauti wa mahitaji kati ya shule moja na nyingine, hasa umbali kutoka Makao Makuu ya Ofisi ya Elimu ya Halmashauri na pia wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Hii imepelekea shule kupatiwa kiwango mfanano cha ruzuku kwa mwanafunzi. Yaani TShs. 10,000 kwa mwanafunzi wa shule za msingi na TShs 25,000 kwa mwanafunzi wa shule za sekondari. Tunayo taarifa kuwa Serikali imekwisha tengeneza na kukipitisha kikokotoo hiki ili kuja na kanuni mpya; hata hivyo imekuwa muda mrefu sasa hakijakaanza kufanya kazi. Ni rai yetu kwa Serikali na Wabunge kuhakikisha kuwa kanuni hii yenye kikokotoo kipya inaanza kutumika Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**Uhaba wa Madarasa**

Utekelezaji wa Elimu bila ada umeongeza idadi ya wanafunzi shule za elimu ya msingi, na unatarajia kuongeza wanafunzi wengi zaidi elimu ya sekondari. Idadi ya wanafunzi kwenye shule za msingi imeongezeka kutoka wanafunzi 8,222,667 Mwaka 2016 hadi 10,024,815 Mwaka 2020, bila Serikali kuwekeza kwa kiwango cha juu kwenye miundombinu, hususan madarasa, ili kukabili ongezeko la wanafunzi 1,802,148. Hali hii imesababisha kuwa na uhaba mkubwa wa madarasa zaidi ya 82,200 (BEST 2020) na hivyo kufanya uwiano wa wanafunzi kwa darasa kuwa 1:75 badala ya kiwango stahili cha 1:45 na hivyo kusababisha mazingira ya ufundishaji kuwa magumu kwenye shule za msingi. Tunatambua kuwa, Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI ya Mwaka 2021/2022 iliyopitishwa imebainisha kukamilisha maboma ya madarasa 3,268 ili kukabiliana na changamoto ya miundombinu kwenye shule za msingi ambayo ni sawa na asilimia 4 tu ya upungufu wa madarasa 82,200. Ili kutatua uhaba wa madarasa kwenye shule za msingi inahitaji uwezekaji mkubwa sana wa takribani TShs trilioni 1.6, na njia pekee ni kuwa na mpango maalumu wa miaka minne kati ya 2021/2022 hadi 2024/2025 kupanga Bajeti ya TShs bilioni 400 kila Mwaka wa Fedha kujenga madarasa 20,000 kila mwaka ili kuondoa uhaba wa madarasa ifikapo Mwaka 2025.

Shule za sekondari zina uhaba wa madarasa 4,647, lakini miaka minne ijayo kuanzia mwaka 2021 hadi 2024 kutakuwa na uhaba mkubwa wa madarasa takriban 41,833 kwa sababu wanafunzi walioongezeka shule za msingi Mwaka 2016 hususan Darasa la Pili na la Kwanza watamaliza elimu ya msingi Mwaka 2021 na 2022. Pia walioanza elimu ya msingi mwaka 2017 na 2018 wanatarajiwa kumaliza Mwaka 2023 na 2024 na kujiunga na Kidato cha Kwanza. Kwa kutumia idadi ya wanafunzi watakaojiunga Kidato cha Kwanza kati ya Mwaka 2021-2024 kutakuwa na ongezeko la wanafunzi takriban mil 1.8 ambapo kwa wastani kila mwaka ongezeko litakuwa wanafunzi 450,000 hivyo watahitaji madarasa 10,000 ambayo yanahitaji kutengewa bajeti ya TShs bilioni 200 kila mwaka kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/2022 na kuendelea kupanga hivyo kwa miaka mingine mitatu hadi mwaka wa fedha 2024/2025. Tunatambua, Serikali kupitia Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI imepanga kujenga shule 300 za sekondari za kutwa kwa mwaka 2021/2022 ili kukabiliana na ongezeko hili. Kimsingi, shule 300 zina uwezo wa kudahili wanafunzi 300,000 endapo kila shule itakuwa na wanafunzi 1,000. Lakini lazima tukumbuke, ongezeko la wanafunzi miaka minne ijayo itafikia hadi wanafunzi mil 1.8 ambayo inahitaji ujenzi wa shule 1,800.

HakiElimu inatoa Rai kwa Serikali kuendelea kuongeza uwekezaji kwenye ujenzi wa madarasa au ujenzi wa shule mpya 450 kila mwaka kuanzia Mwaka wa Fedha 2021/2022 hadi 2024/2025 ili kuzuia wimbi kubwa la wanafunzi kushindwa kujiunga na Kidato cha Kwanza Mwaka 2022. Wakati tukitafakari ongezeko la wanafunzi kwenye shule za sekondari na mahitaji ya madarasa 41,833 kati ya Mwaka 2021-2024, ni muhimu kurejea jinsi uhaba wa madarasa uliyowanyima maelfu ya wanafunzi nafasi ya kuwa shuleni na kujifunza miaka mitatu iliyopita. Mathalani, Mwaka 2018 takribani watoto 133,747 waliohitimu na kufaulu kujiunga na Kidato cha Kwanza walikosa nafasi kutokana na uhaba wa miundombinu. Mwaka 2019 idadi ya waliokosa nafasi ya kujiunga Kidato cha Kwanza kutokana na uhaba wa madarasa ilikuwa ni 21,808 huku Mwaka 2020 idadi hiyo ikiongezeka hadi kufikia 59,765.

**Changamoto ya Uhaba wa Walimu Shule za Msingi na Sekondari**

Kwa mujibu wa Kitabu cha Takwimu za Elimu Tanzania (BEST 2020), shule za msingi zina uhaba wa takriban walimu 50,993. Taarifa ya Waziri wa Fedha ya Mwezi Machi 2021, inaonyesha kuwa katika kipindi cha Julai 2020 hadi Januari, 2021 jumla ya ajira 13,529 za walimu zilitengenezwaa. Ajira hizi zitapunguza uhaba uliopo hadi kufikia 37,464 wa walimu wa shule za msingi. Hata hivyo, uhaba huu bado ni mkubwa na hali halisi mashuleni ni mbaya zaidi kuliko inavyoonekana katika takwimu kwa ujumla. Kwa mujibu wa BEST 2020, bado ikama ya mwalimu kwa mwanafunzi ni changamoto kubwa hasa kwa madarasa ya awali ambayo yana uwiano wa 1: 169 na madarasa ya msingi yenye uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 61 (1: 61) badala ya 1:45.

Serikali na Bunge vinahitaji kuwa na mkakati mahususi wa kupunguza na hatimaye kuondoa uhaba huu unaojitokeza, ili kila mwalimu ahudumie wanafunzi 45 kwa wakati mmoja kama miongozo inavyosema. Hii itasaidia walimu kuwa karibu na wanafunzi na kuwasaidia kwa ufanisi zaidi. HakiElimu tunashauri angalau kila mwaka waajiriwe walimu 18,732 kuanzia Mwa Fedha 2021/2022 ili angalau kuweza kutatua uhaba wa walimu wa shule za msingi ndani ya miaka miwili ya fedha. Tunatambua Mh Rais ameshatoa maagizo ya kuajiri walimu takriban

6,000 lakini bado idadi hii ni ndogo hivyo tunaishauri Serikali kuajiri walimu angalau 18,000 ili tatizo hili litatuliwe. Kwa miaka ya hivi karibuni, uajiri wa walimu umekuwa unafanywa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI lakini katika vipaumbele 23 vya Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI havijataja ajira ya walimu 6,000 kama ilivyoagizwa na mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo, tunatoa Rai agizo hili kutekelezwa na wizara ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Tunatambua na kwa mujibu wa BEST 2020, ikama ya walimu kwa shule za sekondari na hasa kwa masomo ya sanaa ni nzuri. Utaratibu uliotumika Mwaka 2019 wa kuhamisha walimu wa shule za sekondari kwenda shule za msingi katika maeneo ambapo walikuwa wemezidi unaweza kufaa kwa muda mfupi (dharura) tu, hata hivyo kama ufumbuzi wa muda mrefu ni lazima Serikali itenge bajeti ya kuendelea kuajiri walimu wapya waliopungua. Kuna jambo la msingi la kujizingatia kati ya Mwaka 2021-2024 kwani kutakuwa na ongezeko la wanafunzi 1,882,500 ambao wataongeza mahitaji ya walimu takribani 41,833. Kwa kuzingatia ongezeko hili, Serikali inabidi kuanza kuajiri walimu wa shule za sekondari kila mwaka kwa wastani wa walimu 10,458 ili kwa kipindi cha Mwaka 2021-2024 ili kukabiliana na mahitaji ya walimu 41,833.

**Changamoto ya Uthibiti Ubora ya Elimu ya Msingi na Sekondari**

Utekelezaji wa Sera ya 'Elimu Bila Ada' ni wazi kuwa, umekuwa chachu ya ongezeko la udahili shuleni na limepunguza sana changamoto za watoto kuacha shule kutokana na kukosa ada au michango mbalimbali. Kwa mujibu wa BEST 2020, udahili katika ngazi ya elimu ya msingi umeongezeka kutoka asilimia 91.3 Mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 110.3 Mwaka 2019. Kwa ngazi ya sekondari, udahili umeongezeka kutoka asilimia 36 Mwaka 2016 hadi asilimia 43.9 Mwaka 2020, na utaongezeka mara dufu Miaka ya 2022-2024 ambapo wanafunzi wanaojiunga na kKidato cha Kwanza wataongezeka kutoka 562,000 Mwaka 2017 hadi kufikia wanafunzi 1,083,600 Mwaka 2022 na kuendelea kuongezeka hadi kufikia 1,276,100. Hivyo basi ongezeko hili la wanafunzi linatakiwa liende sambamba na mikakati mahususi na mkazo zaidi kwa Serikali kufuatilia utoaji wa elimu, na ubora wake.

Kwa kipindi cha muda mrefu Serikali imeshindwa kuzifikia taasisina shule zote kila mwaka ili kukagua na kuthibitisha ubora wa elimu inayotolewa. Mpaka kipindi cha Mwaka wa Fedha 2017/18 kulikuwa na Wadhibiti Ubora wa Shule za msingi 1,081 tu, wakati mahitaji halisi yalikuwa Wadhibiti Ubora 1,541.Kwa mfano, Mfano Mwaka wa Fedha 2020/21, Serikali, kupitia Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule na Vyuo vya Ualimu ilipanga kufanya ukaguzi na tathmini ya shule za msingi 4,700 badala ya shule 18,152 zilizopo, sekondari 1,200 badala ya 5,072 zilizopo. Hii inamaanisha uwezo wa kukagua shule za msingi na sekondari ni wastani wa asilimia 24-25 ya idadi ya shule zote. Hii inaweza kutafsiriwa kuwa, kwa wastani shule hukaguliwa kila baada ya miaka minne, ilihali ilipaswa ukaguzi ufanyike angalau kila baada ya miaka miwili.

Changamoto hii ya kutofikiwa kwa shule na taasisi za elimu kwa ajili ya ukaguzi na uthibiti wa ubora kunatokana na kutokuwepo kwa bajeti ya kutosha. Mfano katika Mwaka wa Fedha 2018/19 kiasi cha TShs bilioni 1.5 zilitengwa kwa ajili ya kuimarisha shughuli za maendeleo ya uthibiti ubora shuleni, hata hivyo, hadi kufikia Machi 2019 hakuna kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa (Randama Fungu 46 Mwaka 2019). Kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021, kiasi cha TShs bilioni 1 zilitengwa na kuidhinishwa na Bkwa ajili ya kuimarisha shughuli za maendeleo za idara ya uthibiti ubora pamoja na ukaguzi wa shule. Hata hivyo hadi Mwezi Machi 2021, hakuna kiasi cha fedha kilichokuwa kimetolewa. Hii ni changamoto kubwa na ni Rai yetu Bunge na Serikali kuongeza Bajeti ya Maendeleo ya Uthibiti Ubora na pia kuhakikisha fedha iliyopangwa na kupitishwa inatolewa yote ili kusaidia kukamilisha shughuli za ukaguzi wa shule na kuimarisha uthibiti ubora.

Ni Rai yetu kuwa, Bunge na Serikali waangalie namna ya kupanga bajeti ya kutosha kuweza kusaidia shule zote kufanyiwa ukaguzi na uthibiti ubora.

Changamoto ya Elimu ya Mtoto wa Kike.

Pamoja na kwamba mapendekezo yetu yote hapo juu yanawagusa Watoto wote (Ke na Me), kundi la watoto wa kike linahitaji kutiliwa nguvu na mkazo zaidi. Kwa mujibu wa kitabu cha Takwimu BEST 2020, Mwaka 2019 pekee watoto wa kike 1,135 wa shule za msingi waliacha shule kutokana na mimba, huku watoto 5,398 wa shule za sekondari waliacha pia kwa sababu hiyo.

HakiElimu inatambua Azma ya Serikali ya kuhakikisha kuwa ifikapo Mwaka 2025 maeneo yote ambayo ni , wanafunzi wanapatiwa nafasi ya kuishi shuleni kwa maana ya kuwajengea mabweni (TAMISEMI, 2020), na kuwa mpango wa ujenzi wa mabweni haya unaendelea.Hata hivyo, ni vema mpango huu ukawekwa wazi Bungeni na bajeti yake kufahamika. Tunawaomba Wabunge kuhakikisha, wanaomba kupitia na kuidhinisha mpango wa ujenzi huu wa mabweni pamoja na uzio katika shule ambazo zina mwingiliano mkubwa na jamii.

Pamoja na changamoto za ujauzito, elimu ya mtoto wa kike inakabiliwa pia na utoro kutokana na changamoto za 'hedhi' (mtoto wa kike hukosa kati ya siku 3 hadi 4 kila mwezi kutokana na chagamoto hii – SNV 2014), ikichangiwa na mazingira duni ya usafi (sanitation and hygene) shuleni. Vyote hivi kwa pamoja vimesababisha changamoto ya magonjwa na hatimaye utoro kwa idadi kubwa ya watoto wa kike, hasa maeneo ya vijijini.

Ni Rai yetu kwa Wabunge kuendelea kuikumbusha na kuishauri Serikali juu ya umuhimu wa kutenga sehemu ya fedha za ruzuku kwa ajili ya shule kununua taulo za kike ambazo zitakuwa zikigawiwa bure kwa wanafunzi wa kike wenye mahitaji. Hii, itasaidia kuendeleza dhana ya utekelezaji Elimu Bila Malipo na kuondoa vikwazo.

Serikali pia itenge fedha kwa ajili ya kuajiri walimu na watumishi watakaowasaidia kuwapa watoto wa kike na wa kiume elimu kuhusu Afya ya Uzazi. Kwa mujibu wa takwimu za elimu (BEST 2020), idadi ya shule (msingi na sekondari) zilizo na walimu waliopata mafunzo ya Elimu ya Afya ya Uzazi ( Sexual and Reproductive Health and Rights Education) ni 7,517 (42.2%) tu na shule zenye walimu waliopata mafunzo kuhusu Stadi za Maisha kwa ujumla (Life Skills in general) ni 7,757 yaani 43.6% tu ya shule zote.

**3. Hitimisho**

HakiElimu tunafahamu kuwa Elimumsingi ina changamoto nyingi ambazo zinahitaji kushughulikiwa ili kuwezesha upatikanaji wa elimu bora yenye usawa. Hata hivyo, ni muhimu sana kuwa na vipaumbele. Ndiyo sababu, ushauri wetu wa upangaji wa bajeti wa Mwaka wa Fedha 2021/22 umejikita sana katika kutoa kipaumbele kushughulikia changamoto za utoaji Elimu Bila Malipo. Ni muhimu kwa Wabunge na Wizara husika kushughulikia changamoto hizi za kibajeti kama tunataka kutimiza Azma ya kutoa elimu yenye ubora na usawa kwa watoto wote.

**Imetolewa na,**

**Dkt John Kalage**
**Mkurugenzi Mtendaji**

**Tamko hili la bajeti linapatikana pia kwenye tovuti yetu www.hakielimu.or.tz.**





# Wakulima mtama wapewa angalizo kilimo cha mkataba

**Na Renatha Msungu,** KONGWA

WAZIRI wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, amewataka wakulima wa kilimo cha mkataba cha zao la mtama kuzingatia mkataba waliyoingia na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) ili kilimo hicho kiwe na tija.

Katika mkataba huo, wakulima hao watauza kilo moja ya mtama kwa Sh. 550 badala ya bei ya awali ya Sh. 300, kabla hawajaingia mkataba.

Akizungumza kwenye ziara ya kutembelea kilimo cha mkataba cha wakulima hao, Prof. Mkenda alisema kupitia mkataba huo wakulima wanawezeshwa vizuri mbegu, kulima vizuri pamoja na utaalamu likiwamo soko.

"Nawaomba wakulima kuheshimu mkataba mnaokwenda kupewa na TBL, kwa sababu wizara inatunga sheria ya kumlinda TBL pamoja na wakulima ili wasijegeuka na kukataa kuwauzia mazao kipindi cha mavuno kampuni iliyowawezesha," alisema.

Alisema kilimo hicho kitasaidia kuwainua wakulima kiuchumi.

"Hivi sasa wakulima wana uhakika na soko kutoka kwa TBL ambao wameingia nao kufanya kilimo cha mkataba, hivyo ni vema wakatumia nafasi hiyo kujipanua katika kilimo hicho cha mtama

wanachofanya," alisema.

Alibainisha kuwa kero iliyopo kwa wakulima ni kulima kwa wingi lakini hawana uhakika wa mvua wala soko, lakini wakazi wa Kongwa wamepata bahati ya kuendesha kilimo cha mkataba na TBL.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sagara 'B', Gilbert Mlwande, alisema hatua hiyo imesaidia kwa kiasi kikubwa kuwainua wakulima wa zao hilo kiuchumi.

Kwa upande wake, Mwakilishi kutoka TBL, Mesiya Mwangoka, alisema TBL inaendelea kutafuta wakulima wa zao hilo katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo

ili kufanikisha kile walichokusudia katika kilimo cha mtama.

Alisema lengo la TBL ni kuhakikisha wakulima wanafanikiwa na TBL nayo inafanikisha kupata wakulima ambao watalima kilimo hicho kwa ufasaha na kupata mazao mengi.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, akizungumza na wananchi wa eneo la Mbande, wilayani Kongwa, Mkoa wa Dodoma. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# CHAWATA yataka bajeti inayowagusa watu wenye ulemavu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHAMA cha wenye Ulemavu Tanzania (CHAWATA) mkoani Dodoma, kimeliomba Bunge kupitisha bajeti ambazo zitawagusa watu wenye ulemavu.

Rai hiyo ilitolewa na Katibu wa CHAWATA mkoa wa Dodoma, Kelebi Mhawi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma, ambapo ameliomba Bunge kuhakikisha katika bajeti wanazopitisha wahakikishe zinaigusa jamii hiyo.

Katibu huyo alisema kuwa mara nyingi watu wenye mahitaji maalumu wamekuwa wakisahaulika kwenye bajeti na hasa katika huduma za kijamii na kusababisha kushindwa kuondokana na umaskini unaowakabili wenye ulemavu walio wengi.

Alisema, sehemu ya huduma ambazo watu wenye ulemavu, wanazosahaulika ni upatikanaji wa huduma za afya, visaidizi, fimbo nyeupe, viti mwendo na dawa kwa ajili ya wenye ualbino.

Alisema kuwa hali hiyo ya kusahaulika pia ipo katika bajeti ambayo inayoweza kuwawezesha kufanya uendeshaji wa vyama vya watu wenye ulemavu nayo haipo pamoja na sheria inawataka kufanya hivyo.

"Hivyo tunaliomba Bunge letu tukufu kuhakikisha wanapopitisha bajeti zao ziwaguse hawa watu wenye ulemavu, ili na wao waweze kujimudu kwenye maisha yao kama ilivyo kwa wengine wasiokuwa walemavu," alisema.

Hata hivyo, Katibu huyo wa CHAWATA aliwaomba wabunge kufanya kazi iliyowapeleka ya kupitisha sheria na bajeti ili fedha zitoke zikatoe huduma mbalimbali kwa wananchi kama ilivyokusudiwa.

# Aweso akemea makadirio ya juu ujenzi wa miradi ya maji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, amekemea tabia ya wataalamu wanaofanya makadirio ya miradi ya maji kuacha kuweka makadirio ya juu ya ujenzi ili kulisaidia taifa kutatua kero za maji.

Waziri Aweso aliyasema hayo mwishoni mwa wiki jijini hapa, alipokuwa akifunga kikao cha majadiliano ya wataalamu wa sekta ya maji kutoka Tanzania Bara na Visiwani.

Alisema wizara ilifikia miradi 192 nchi nzima, ambayo ilikadiriwa kutumia Sh. bilioni 207, lakini kutokana na kutumia wataalamu wa ndani imetumia Sh. bilioni 163 na kuokoa Sh. bilioni 44.

"Mradi wa Matamba Kinyika Wilaya ya Makete ambao ni mradi wa vijiji saba, ulikadiriwa kujengwa kwa Sh. bilioni 4.7, lakini ulijengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 1.5, hivyo kuokoa zaidi ya Sh. bilioni tatu," alisema.

Alisema kuna umuhimu wataalamu hao kuwa wazalendo kwenye ukadiriaji ili kusaidia fedha inayopatikana kutumika kutatua kero ya maji maeneo mengine.

Pia, aliagiza kila jumuiya ya watumiaji maji kuwa na mtunza fedha na msimamizi ili inapotokea marekebisho, yafanyike na miradi iwe endelevu.

Hata hivyo, alisema bado jamii ina uelewa mdogo juu ya ulipaji wa ankra za maji na kutaka waelimishwe walipe, lakini zisiwe za kubambikiziwa.

"Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza suala la wananchi kupata huduma za maji, lakini wavilinde vyanzo vya maji visipotee," alisema.

Alisisitiza mikakati ya kuongeza vyanzo vya

maji na kuwataka wataalamu kutumia utaalamu wao kuchimba mabwawa na kuonanamna bora ya kuvuna maji ya mvua ambayo mengi hupotea ardhini.

"Wataalam lazima kujipanga na kuvuna maji, mnatakiwa kutengeneza mikakati ya kuongeza vyanzo vya maji kupitia Wizara ya Maji kuna mabonde tisa yakiwamo Wami, Ruvu, Victoria, Nyasa na mengine ambayo

yapo mahsusi kwa ajili ya kulinda na kutunza vyanzo vya maji," alisema.

Katibu Mkuu wa Maji, Nishati na Madini kutoka Zanzibar, Muingereza Miraji Mzee, alisema ushirikiano katika utekelezaji wa miradi ya maji utaleta matokeo chanya.

Naye, Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Mhandisi Anthony Sanga, alisema hakutakuwa na mchezo kwenye utekelezaji wa miradi ya maji, hivyo wataalamu wanapaswa kujipanga kuhakikisha miradi inakwenda kama iliyopangwa.



## Wawekezaji Mbeya watakiwa kuzingatia sheria

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya, imewataka wawekezaji wa kigeni waliopo mkoani humo kufanya kazi zao kwa kuzingatia sheria za nchi ili wafanye kazi zao bila usumbufu unaoweza kusababishwa na wao kukinzana na sheria za nchi.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, mwishoni mwa wiki wakati wa kikao maalumu kati ya Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa huo, Kituo cha Uwekezaji nchini (TIC) na wawekezaji wenye asili ya China.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki kwa ajili ya wawekezaji ili kuwawezesha kufanya kazi zao kwa utulivu na kuchangia kupunguza tatizo la ajira na kuinua uchumi wa nchi.

"Rais wetu Samia Suluhu Hassan, amesisitiza wawekezaji kupewa kipaumbele, sasa mimi nataka niwahakikishie kwamba katika mkoa wetu huu hakutakuwa na mkwamo wa aina yoyote ile, tumejipanga na wenzetu wa TIC pamoja na vyombo vya dola ili kusiwepo na matatizo," alisema Chalamila.

Alisema moja kati ya sheria ambazo wawekezaji wanatakiwa kuzingatia wakati wa uendeshaji wa kazi zao ni sheria ya kazi ambayo inasisitiza mikataba na mambo mengine ya kuzingatia wakati wa kutoa ajira.

Kwa upande wao baadhi ya wawekezaji hao waliishukuru serikali kwa kuwapatia ufafanuzi huo huku wakilazimika kuomba radhi kwa serikali na Watanzania kutokana na tukio la hivi karibuni la mwenzao mmoja kumcharaza bakora mmoja wa Watanzania mkoani Mbeya.

Yang Si Yu ambaye ni mmoja wa wawekezaji katika mkoa huo, alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zina mazingira mazuri ya uwekezaji na kuahidi kuendelea kuwekeza kwenye shughuli mbalimbali.

Alisema tukio la mwenzao kumshambulia Mtanzania halikuwafurahisha hata wao na kuomba waendelee kuvumiliana.

Kwa upande wake Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, Ulrich Matei, alisema jukumu la jeshi hilo ni kuhakikisha wawekezaji wanaishi kwa amani.

# Wataka kukutana na TANAPA kukomesha mauaji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

SIKU chache baada ya watu watatu kukutwa wameuawa na miili yao kutupwa ndani ya maji katika Mto Ruaha Mkuu, Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali limetaka kukutana na uongozi wa Hifadhi za Taifa nchini (TANAPA) ili kujadili namna ya kukomesha mauaji yanayotokea mara kwa mara ndani ya hifadhi.

Hoja hiyo ilitolewa juzi kwenye kikao cha kawaida cha baraza hilo na Diwani wa Kata ya Chimala, Charles Komba, akisema wanastahili kutoa tamko la pamoja kuhusu mauaji hayo.

Komba alisema kuwa suala la mauaji limekuwa likitokea mara kwa mara ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na mara zote askari wa TANAPA ndio wamekuwa watuhumiwa wa mauaji hayo na hakuna hatua zinazochukuliwa za kukomesha mauaji ya aina hiyo.

Alisema kwa kipindi cha miaka minne yameshatokea mauaji ya watu zaidi ya 12 ndani ya hifadhi hiyo yakihusisha wananchi wa Wilaya ya Mbarali na wengi wao wakiwa ni wa jamii ya wafugaji.

"Matukio ya watu kuuawa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha ndani ya halmashauri yetu ya Mbarali yamekuwa yakitokea na kujirudia mara kwa mara, sio busara baraza hili kuendelea kukaa kimya, nashauri tujigeuze kama kamati tujadili mauaji haya na kutoa tamko ambalo litasaidia wananchi wetu kuishi salama na kwa amani," alisema Komba.

Hata hivyo, ombi hilo lilileta mjadala wa kikanuni ulioibua mvutano baina ya menejimenti na madiwani kuhusu baraza hilo kujigeuza kuwa kamati ya kujadili suala hilo. Upande wa menejimenti ulidai kuwa kanuni zinaruhusu baraza hilo kujigeuza kuwa kamati kwa lengo la kujadili nidhamu ya watumishi pekee na sio suala lingine nje ya nidhamu na mwenendo wa watumishi.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alisema kuwa hoja iliyoletwa ijadiliwe ni ya kiusalama na hastahili kujadiliwa na baraza hilo kwa madai kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vinaendelea kulishughulikia.

"Hakuna anayependa mambo ya mauaji yatokee kwenye wilaya yetu, hili ni suala la kiusalama na vyombo viko kazini kulishughulikia, hivyo haitakuwa vizuri suala ambalo linachunguzwa na vyombo vya dola likaendelea kujadiliwa hapa," alisema Mfune. Kauli hiyo ilisababisha Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali, Twalib Lubandamo, kusitisha mjadala huo, lakini alisema ipo haja ya Mkuu wa Wilaya kuwakutanisha askari wa TANAPA na Baraza la Madiwani ili wajadili kwa pamoja namna ya kukomesha mauaji ndani ya hifadhi hiyo.

"Suala hili la mauaji limekuwa likitokea na kujirudia mara kwa mara, haiwezekani sisi madiwani ambao tumeaminiwa na wananchi tukae kimya kwani tutakuwa hatuwatendei haki wananchi waliotuamini, hivyo naomba kabla ya kutoa tamko letu tukutane na hao wenzetu wa hifadhi ili tuzungumze nao," alisema Lubandamo.

Aprili 26, mwaka huu, watu watatu walikutwa wameuawa na miili yao kutupwa majini ndani ya Mto Ruaha Mkuu, watu wawili kati yao miili yao ilipatikana na mtu wa tatu alipatikana kichwa kisichokuwa na kiwiliwili.

Aidha, watu wengine watatu ambao wanadaiwa walikuwa pamoja na watu hao waliouawa, hawajulikani walipo mpaka sasa na kufanya idadi ya watu wanaohofiwa kuuawa ndani ya hifadhi hiyo kuwa sita.



Gari likipita kwenye dimbwi la maji kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha na kuharibu barabara katika eneo la Kitunda Kivule jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Wahakikishiwa stahiki, mazingira bora ya kazi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, Twalibu Lubandamo, amewahakikishia watumishi kushughulikia vikwazo vinavyowakabili ikiwamo kupata stahiki zao kwa wakati pamoja na kuboreshewa mazingira ya kazi.

Lubandamo alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na Nipashe kuhusu walivyojipanga kutatua vikwazo vya wafanyakazi ikiwa ni siku chache tangu kufanya maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi Duniani.

Alisema watumishi wanajitahidi kufanya kazi kwa ari na moyo bila kujali vikwazo wanavyokabiliana navyo na njia pekee ya kulipa fadhila na kuwaandalia mazingira rafiki kwao ili kutimiza majukumu ipasavyo.

"Nawapongeza watumishi kwa kazi kubwa mnayoifanya katika kuwatumikia wananchi, hakika tumeona mabadiliko na maendeleo kwenye maeneo yetu kuanzia sekta ya elimu, afya, kilimo na maendeleo ya jamii bila kuwasahau watendaji wa vijiji na kata wamekuwa kiungo kikubwa kati ya serikali na wananchi," alisema Lubandamo.

Alisema walimu wana mchango mkubwa katika kuleta maendeleo wilayani humo kwa kujjitahidi kuongeza ufaulu siku hadi siku, lakini kuandaa vijana kujitegemea.

Alisema moja ya masuala ambayo Baraza la Madiwani wa Halmashauri hilo linafanya ni kuendelea kuboresha miundombinu ya elimu kwa kuhakikisha wanafunzi wanakaa kwenye madawati, vifaa vya kujifunzia na kufundishia, walimu wa kutosha pamoja na miundombinu ya madarasa na nyumba za walimu.

Pia kuendelea kutoa motisha kwa walimu wanaofanya vizuri ili waendelee kufanya vizuri na kuongeza ufaulu wilayani Mbarali.

Diwani wa Kata ya Imalilo Usongwe, Chuki Mbwajine, ambaye aliandaa hafla ya kuwapongeza watumishi hususani walimu kwa kazi kubwa wanayoifanya, alisema lengo ni kuwaunganisha pamoja kujadili vikwazo wanavyokabiliana navyo na namna ya kutatua.

Alisema hafla hiyo imeakuwa chachu ya kuleta mabadiliko katika kata hiyo ikiwa ni pamoja na kuongeza ufaulu, wananchi kupewa elimu ya kilimo na ufugaji wa kisasa.

Baadhi ya walimu walipongeza jitihada zinazofanywa na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali katika kuwatetea na kujali maslahi yao.

Aidha, walipongeza hotuba ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kupunguza baadhi ya tozo ambazo zilikuwa zikiwaumiza wafanyakazi.





# SMZ yarejesha taasisi zenye uwezo mdogo kwenye wizara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imeamua kuzirejesha kwenye wizara zake taasisi zilizogatuliwa kutokana na uwezo mdogo wa mabaraza ya manispaa na halmashauri kuzihudumia taasisi hizo.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, aliyasema hayo katika hafla ya utiaji saini makabidhiano ya taasisi hizo katika ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil Mjini Zanzibar.

Alisema awali lengo la serikali kuzigatua taasisi hizo ni kuimarisha utoaji wa huduma bora kwa wananchi, lakini tathmini iliyofanywa imeonesha kujitokeza changamoto ya ukubwa wa majukumu.

Alisema changamoto hizo zinatokana na kuongezeka kwa vyumba vya kusomea shuleni, kuongezeka kwa vituo vya afya na kushuka kwa kiwango cha elimu na huduma za afya. Akiyataja majukumu yaliyoondolewa katika ugatuzi ni elimu ya msingi ambayo itatekelezwa chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Afya msingi chini ya Wizara ya Afya Ustawi wa jamii, kilimo ambayo imerejeshwa Wizara ya Kilimo na baadhi ya maeneo ambayo yamerejeshwa katika wizara ya uchumi wa buluu.

Waziri Masoud alisema kwa upande wa barabara za ndani zilizokuwa zikitekelezwa chini ya ofisi yake kupitia fedha ya mfuko wa barabara nayo imerejeshwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

"Wizara hizo zitaendelea kubeba jukumu kama ilivyokuwa awali Wizara ya Elimu itaendelea kubeba jukumu la elimu kwa eneo lote kuanzia msingi na kuendelea, Afya, Kilimo na Wizara ya Miundombinu," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali imeamua watumishi wote waliopelekwa katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, kwenda kutekeleza majukumu yao ya kisekta watarejeshwa katika wizara husika walizokuwa wakifanyia kazi awali.

"Walimu wataendelea na majukumu yao chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, watoa huduma za afya watakuwa chini ya wizara yao ya afya ustawi wa jamii na watendaji wa Wizara ya Kilimo na watendaji wa barabara nao hivyo hivyo," alisema.

Alisema huduma zitaendelea kutolewa kama kawaida na kuongeza ufanisi huku serikali ikiendelea kutathmini zaidi ya kuamua hapo baadaye na kuahidi kuwa utoaji wa huduma hautoathirika.

Alisema uamuzi huo utaanza kutekelezwa rasmi kuanzia mwaka wa fedha ujao wa 2021/2022 katika mafungu ya bajeti yakiwamo majukumu ya utekelezaji wa shughuli hizo pamoja na mishahara ya watumishi hao yatakwenda katika wizara husika zilizotajwa.

Pia, serikali itaendelea kuwa karibu na wananchi na kuamini kwamba changamoto zilizokuwa zikijitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu chini ya mfumo huo zitaondoka.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhammed Said, alisema licha ya uamuzi huo wa serikali, wizara anayoiongoza itaendelea kushirikiana na wakuu wa mikoa, wilaya, Baraza la Mji na halmashauri ili kuweka mazingira bora ya elimu.



Wakazi wa Mkoa wa Kusini Unguja wakijumuika na mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi, katika futari maalum iliyoandaliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (hayupo pichani), katika ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein (SUZA) Tunguu Wilaya ya Kati Unguja. **PICHA: IKULU**

# Ofisi ya Mufti yaridhishwa misaada kwa wasiojiweza

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

OFISI ya Mufti wa Zanzibar imeeleza kuridhishwa na sadaka zinazotolewa kwa watu wenye mahitaji maalum na watoto yatima ambayo inasaidia kuimarisha amani, upendo na kupunguza ukali wa maisha miongoni mwa jamii.

Katibu wa ofisi hiyo, Shekhe Khalid Ali Mfaume, alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza wakati wa shughuli ya ugawaji wa vyakula vya futari iliyotolewa na Taasisi ya Shura Muslim Charitable Organization katika ofisi za jumuiya hiyo, Kilimahewa, mjini Zanzibar.

Alisema Mwenyezi Mungu aliyataja makundi ya yatima, wajane na watu wasiojiweza kuwa miongoni mwa yanaopaswa kusaidiwa na jumuiya hiyo imefanya jambo jema linalopaswa kuigwa na kila mwenye uwezo.

"Tumehimizwa na Allah (S.A.W) kuwashika mkono mayatima, maskini na wale wenye mahitaji maalum kwani kufanya hivyo sio kunawapunguzia ugumu wa maisha tu, bali huongeza upendo na kujenga amani katika jamii," alisema Shekhe Mfaume.

Alisema jamii isiyokuwa na usawa, watu wake wanakosa utulivu wa nafsi na kuwa sababu ya kuoneana choyo na husda na kwamba ipo haja kwa kila mmoja kujenga utamaduni wa kutoa sadaka kwa kadiri ya uwezo alionao.

Aliwashukuru wafadhili wa jumuiya hiyo, Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu (UAE) kwa kufadhili futari na shughuli za jumuiya hiyo ambayo imekuwa ikitoa misaada mbalimbali ikiwamo ya elimu kwa watoto yatima.

Naye Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo, Juma Ali Khamis, alisema jumla ya msaada huo ni mwendelezo wa misaada inayotolewa na jumuiya yake kwa familia zinazolea watoto yatima, wazee na watu wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Kadhalika kabla ya kutoa msaada wa futari kwa wananchi wa Unguja, walifanya hivyo katika maeneo mbalimbali ya kisiwa cha Pemba pamoja na kufutarisha katika maeneo ya Unguja na zaidi ya watu 4,000 wamenufaika.

"Toka jumuiya yetu ilipoanzishwa mwaka 2014 tumekuwa na harakati zinazoyahusu makundi haya na kwa mwaka huu Alhamdulillah tulianza kwa kutoa sadaka ya vyakula vikavu kule Pemba na sasa tupo hapa Unguja," alisema Maalim Juma.

Kwa upande wake, mmoja wa wanufaika wa sadaka hiyo anayetunza watoto saba mayatima wakiwamo wanawake wanne, aliwashukuru wafadhili waliofanikisha kupatikana kwa sadaka hiyo na viongozi wa jumuiya ya Shura kwa kuwapatia msaada huo ambao alisema utawasaidia kupunguza ugumu wa maisha.

"Tunashukuru vyakula hivi vitatusaidia kupata utulivu katika masuala ya chakula katika kipindi hiki cha Ramadhani na kile kipato kidogo tulichonacho tutakitumia kwenye masuala ya mavazi ingawa bado tunaomba tusaidiwe na huko," alisema mama huyo ambaye hakutaka kutajwa jina lake.

Katika hafla hiyo zaidi ya familia 150 zinazoishi na watoto yatima, wazee wasiojiweza na wanaoishi kwenye mazingira magumu walipatiwa futari hiyo iliyojumuisha mchele, maharagwe, mafuta ya kula, sukari, unga wa ngano na tende.

# ZAECA yahakikisha kutenda haki kwa kila mtu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), ACP Ahmed Khamis Makarani, amesema taasisi yake imejipanga ili kuhakikisha kazi inafanyika bila ya kumwonea mtu muhali.

Alisema kuna baadhi ya wananchi wanadhani kuwa viongozi wao hawaguswi kuwachukulia hatua pale wanapokamatwa na rushwa kwa kutumia madaraka yao vibaya.

Alisema jambo hilo halipo kila mtu atahukumiwa kwa mujibu wa sheria na kosa lake.

Mkurugenzi Mkuu huyo alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari, makao makuu ya taasisi hiyo mjini hapa.

Alisema katika kuhakikisha kuwa taasisi hiyo inafanya kazi hivi sasa wako katika mpango wa kuzitizama kero zote zilizowasilishwa katika taasisi hiyo ili kupelekwa mahakamani kwa mujibu wa sheria ya rushwa.

Alisema katika mapambano ya kuzuia rushwa ni lazima wananchi nao wawe tayari kwa kutoa ushahidi pale mtuhumiwa anapopata kesi ya rushwa.

Alisema lazima jamii iwe tayari katika kutokomeza rushwa na muhali kwa vile imekuwa adui kwa maendeleo ya Taifa la Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,
Chenye Thamani Kubwa
Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa
Tupigie 0782253676**

**RE: THE LAND ACT NO 4 OF 1999
LOSS OF ORIGIONAL LETTER OF OFFER
OF
REF NO: MMC/LD/21630
REGISTERED OWNER: YUSTO ONESMO
LAND: PLOT NO. 18 BLOCK 'K' KIHONDA AREA
MOROGORO MUNICIPALITY
APPLICANT: YUSTO ONESMO**

**TAKE NOTICE** that the **ORIGIONAL LETTER** OF OFFER to the land described above is said to be lost and that I intended to issue a **REPLACEMENT OF THE ORIGIONAL LETTER OF OFFER** in lieu thereof unless cause to the contrary is shown within thirty (30) days from the date of this publication.

The **ORIGIONAL LETTER OF OFFER** if found, should be delivered to the office of the; Municipal Director , Morogoro Municipal Council, **P.O.Box 166 Morogoro.**

**Issued by:**

**For: MUNICIPAL DIRECTOR
MOROGORO**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
ILIYOPO MOROGORO
TANGZAZO LA KUITWA SHAURINI
SHAURI LA MADAI/TARAKA/MIRATHI NAMBA: 71/2021
MADAI/MUOMBAJI/MSIMAMIZI: BARAKA MUSSA KASONTA
DHIDI YA
MDAIWA: ALLY SALUM MGAGALA
KWA: ALLY SALUM MGAGALA
OMBI LA MDAI/MUOMBAJI/MSIMAMIZI
BARAKA MUSSA KASONTA**

MADAI YA : MADAI YA PESA TSH 2,000,000/=
Unatakiwa kuhudhuria hapa mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa . Shauri limepangwa kusikilizwa mnamo tarehe 11 mwezi 5 mwaka 2021 saa 2:00 Asubuhi.

Angalia kama *kuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu. Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 29 mwezi 4 mwaka 2021

**HAKIMU
MAKA MA YA MWANZO MJINI
MOROGORO**

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

KAMPUNI YA DEEPAK'S LIMITED Uongozi na wamiliki wa Kampuni ya DEEPAK'S LIMITED yenye namba ya usajili 10109, iliyopo plot namba 1280, block namba 84, Zanaki Street, iliyosajiliwa mwaka 1984 wameamua kwa hiyari yao kuifunga Kampuni.

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

MAKAJI JUMA ABDALA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SANLG YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 808 BGA YENYE CHASIS NA.LBRSPJB50G9008510 NA ENGINE NA.16912713.TAARIFA IMETOLEWA KATIKA KITUO CHA POLISI MASWA NA.MAS/B.1/6/VOL XV/34.

## UPOTEVU WA KADI ZA MAGARI

GUO QBING CHINESE ENGINIARIN inatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili T 478 AAG – MITSUBISHI. CHASSIS No. FV415J-A43603. T 258 AYG – MITSUBISH. CHASSIS FV 415J-A42798. T 658 AAG – MISTSUBISH. CHASSIS No. FV 415J-A42804. T 576 AGY – DONG FANG. CHASSIS No. D.FH180. KWA YEYOTE MWENYE TAARIFA APELEKE KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU NAYE. TAARIFA YA POLISI: MBE/MBE/RB205391/2021.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika Mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi
NO.129/2021**

Ombi la **MWAMVUA MAFTAH AHMED** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **MAFTAH AHMED SALANGA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 07/06/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe03/05/2021**

**Uza,
Chenye Thamani
Kubwa Kwa
Kutangaza Nasi
Kwa Bei Poa
Tupigie
0782253676**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KITAIFA

# Wanahabari watakiwa kujadili zaidi vikwazo

**Na Elizabeth Zaya**

WADAU wa habari, wamesema kuna haja wanataaluma wote katika sekta hiyo kuungana kuendelea kujadili changamoto mbalimbali zinazoikabili tasnia hiyo nchini.

Wadau hao walitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wakijadili hotuba ya hivi karibuni ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu uhuru wa vyombo vya habari nchini.

Pamoja na mambo mengine, wadau hao kutoka vyombo mbalimbali vya habari nchini, walijadili na kupitia sheria zinazosimamia sekta hiyo.

Katibu Mtendaji wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena, alisema hotuba ya hivi karibuni ya uhuru wa vyombo vya habari ya Rais Samia, ilionyesha matumaini makubwa kuhusiana na mustakabali wa uhuru kwenye tasnia hiyo nchini.

Meena alisema kwa kipindi kirefu, wadau wa habari nchini, wameishi katika giza nene, lakini kupitia hotuba ya hivi karibuni ya Rais Samia, tayari wameanza kupata mwanga na matumaini makubwa.

Alisema ili tasnia hiyo iendelee kubaki kuwa miongoni mwa sekta zinazoheshimika, kuna haja ya wadau hao kufanya kazi kwa umoja ikiwamo kuendelea kutetea haki zao.

Pia aliwakumbusha wadau hao kuhakikisha kwamba wanafanya kazi kwa weledi na kuzingatia maadili ya kazi yao.

"Na miongoni mwa vitu vya kuendelea kuvipigania hususani tunapoadhimisha siku ya uhuru wa vyombo vya habari ni pamoja na mamlaka kuhakikisha zinatambua kwamba zina kazi ya kulinda haki za waandishi wa habari nchini," alisema Meena.

Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA-Tan), Salome Kitomari, alisema hotuba iliyotolewa na Rais Samia, ina maana kubwa kwa mustakabali wa uhuru wa vyombo habari nchini na wanaamini kwamba huenda ikawa na matokeo chanya kwa sekta hiyo.

Salome alisema pamoja na hayo, bado kunahitajika nguvu kubwa katika kulinda taaluma na haki za waandishi hao wa habari nchini.

Kaimu Mwenyekiti wa Wamiliki wa Vyombo vya Habari Tanzania(MOAT), Samwel Nyalla, alisema kuna haja ya wadau hao wa habari kukaa pamoja kujadili mambo ya msingi na kubainisha changamoto zilizopo katika sekta hiyo ili kuziwasilisha kwenye mamlaka husika serikalini kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

# Safari za ATCL China moja kwa moja J'mosi kwa masharti

**Na Romana Mallya**

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL), Mhandisi Ladislaus Matindi, amesema shirika hilo litaanza kufanya safari za moja kwa moja kati ya Dar es Salaam (Tanzania) na Guangzhou (China) kuanzia Jumamosi kwa masharti ya kusafirisha raia wa nchi hiyo na wenye vibali maalum.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, Mhandisi Matindi, alisema safari hizo zinafanyika kwa kufuata masharti waliyopewa na China ikiwa ni katika kukabiliana na janga la virusi vya corona.

Alisema wasafiri watakaotoka Tanzania kwenda China, watatakiwa kupima afya zao mara tatu kabla ya safari ili kujihakikishia hawana maambukizi ya corona.

"Masharti tuliyopewa ni pamoja na safari ya kuelekea mji wa Guangzhou itafanyika mara moja kila baada ya wiki mbili badala ya wiki moja tulizoomba, ndege itaondoka Dar es Salaam Jumamosi saa 11 alfajiri na itawasili mjini Guangzhou saa 3 usiku na itaanza safari yakurejea Tanzania saa 5 usiku na kuwasili Dar es Salaam saa 11alfajiri siku ya Jumapili," alisema.

Alitaja masharti mengine ni wakati ndege inakwenda China abiria watakaoruhusiwa kwa safari hizo ni raia wa China, ni wa nje wenye vibali maalum na wale wenye vibali vya makazi.

Alisema wakati ndege inarejea Tanzania hakutakuwa na masharti hayo.

Mhandisi Matindi alifafanua kuhusu vipimo vya corona na kueleza kuwa wasafiri watapima corona mara tatu kabla ya safari ambapo Jumatano na Alhamisi watapima kipimo cha PCR na Ijumaa kitafanyika cha IGM na ambao hawatakutwa na maambukizi watapeleka majibu yao Ubalozi wa China na ndipo shirika hilo litakapowapatia tiketi.

Alisema kabla msafiri hajaingia kwenye ndege atafanyiwa kipimo cha PCR na baada ya hapo ndipo ataruhusiwa.

Alisema mashirika ya ndege likiwamo la Tanzania yamepewa masharti na China kuwa endapo wakienda na abiria watano au zaidi wenye corona nchini humo shirika husika litafungiwa kwa miezi miwili kufanya safari nchini humo.

Kuhusu usafirishaji wa mizigo, alisema hakuna masharti yoyote waliyopewa kutokana na corona na kuwataka wafanyabiashara kutumia fursa hiyo.

Alisema uuzaji wa tiketi utafanywa na mawakala watatu wa China.




Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kifuru, jijini Dar es Salaam, wakivuka barabara jana, huku magari yakiwasubiri ikiwa ni sehemu ya utii wa sheria za usalama barabarani. **PICHA: SABATO KASIKA**

# RAS ataka mafunzo ya PPRA kuwa tiba usimamizi mikataba

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Tawala Mkoa wa Mara, Karoline Albert Mthapula, amewakaribisha katika mkoa huo wawezeshaji wa mafunzo ya sheria ya ununuzi wa umma kutoka Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), akieleza kuwa anaamini elimu watakayoitoa itakuwa sehemu ya suluhisho la changamoto ya usimamizi wa mikataba ya ununuzi.

PPRA inatoa mafunzo ya sheria ya ununuzi wa umma na mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS) kwa watendaji wa taasisi za serikali za mkoa huo. Mafunzo hayo ya siku tatu (Mei 3-5) yanatolewa bure kwa washiriki 80.

Akizungumza na wawezeshaji hao waliomtembelea ofisini kwake jana, Mthapula alisema watendaji wa mkoa huo wana changamoto hasa katika usimamizi wa mikataba ya ununuzi unaotumia 'force account', na kwamba maeneo yanayowapa shida zaidi ni pamoja na jinsi ya kutofautisha mkataba wa 'local fundi' na mkataba wa mkandarasi.

"Tunahitaji kuwa na usimamizi wenye ukamilifu ili uwe mfano kwa wengine hasa katika halmashauri zetu, naamini kwa mafunzo haya mtatusaidia," alisema Mthapula.

Aidha, alisema kukosekana kwa elimu ya ununuzi wa umma hasa kwa watendaji wanaofanya kazi maeneo ya vijijini kumesababisha matatizo ya usimamizi ambayo yangeweza kuepukika.

"Kwa hiyo, ni muhimu kuwa na elimu kwa sababu bila elimu ni changamoto. Ninaomba na ninatamani elimu hii iwafikie wahusika wa kamati zote na watendaji wote katika mkoa wetu," aliongeza.

Naye Mkurugenzi wa Kujenga Uwezo na Ushauri kutoka PPRA, Mhandisi Mary Swai, alimshukuru Katibu Tawala huyo kwa kuwakaribisha na kueleza kuwa anaamini baada ya mafunzo watakayoyatoa washiriki wataongeza ufanisi katika usimamizi wa mikataba. Hivyo, alisema yataongeza ukidhi na upatikanaji wa thamani ya fedha kwenye ununuzi wa umma.

Watumishi wa PPRA waliomtembelea Katibu Tawala wa Mkoa wa Mara ofisini kwake, pamoja na Mhandisi Swai, wengine ni Gloria Mboya (Meneja Rasilimali Watu), Frank Yesaya (Ofisa Ununuzi) na Joseph Muhozi (Ofisa Uhusiano kwa Umma).

## HABARI MICHEZO



# BALE: NAFURAHIA KUCHEZA TENA SOKA

**LONDON,** England

GARETH Bale amesema sababu kubwa ya yeye kuimarika kwa kiwango chake ni kuchezeshwa mara kwa mara tangu Ryan Mason achukue mikoba ya Jose Mourinho kama kocha wa Tottenham Hotspur.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales alifunga 'hat-trick' yake ya pili kwenye Ligi Kuu England na ya kwanza tangu Desemba 2012, wakati Tottenham ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Sheffield United, Jumapili.

Alitolewa kipindi cha pili wiki iliyopita kwenye fainali ya EFL ya kipigo kutoka kwa Manchester City, lakini straika huyo ameanza kwenye mechi zote za ligi chini ya Mason, akifunga mabao manne kwa ujumla.

Na hiyo inalinganishwa na mabao matano katika mechi 14 chini ya Mourinho kwenye Ligi Kuu msimu huu, sita kati yake akianza.

Na Bale, ambaye anajiandaa kurudi kwa klabu yake ya Real Madrid mwishoni mwa msimu huu kumalizia mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake, anajisikia tena fahari kufurahia soka.

"Unatakiwa kuchukua nafasi yako wakati zinapokuja, hivyo najisikia vizuri," alisema akiiambia Sky Sports.

"Nilikuwa nataka tu kucheza mechi na kuweza kufanya kile unachokitaka na ndicho nitakachokifanya sasa. Nina furaha na nina furaha sana kucheza vizuri.

# Hakimi azungumzia kurudi Real

**MILAN,** Italia

ACHRAF Hakimi, amesema alipenda kubaki kule Real Madrid baada ya kusherehekea taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, akiwa na Inter Milan, ingawa ameacha mlango wazi kwenye uwezekano wa kurudi.

Hakimi alijiunga na Inter akitokea Madrid mwanzoni mwa msimu huu kwa ada iliyoripotiwa kuwa euro milioni 40, na Jumapili mlinzi huyo wa pembeni aliongeza taji la Scudetto kwenye medali zake.

Inter walitawazwa kuwa mabingwa wapya wa Italia kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2009-10 baada ya Atalanta kutoka sare ya bao 1-1 na Sassuolo na kuwaacha Nerazzurri wakiongoza kwa pointi 13 zaidi kileleni ambazo hakuna timu inayoweza kuzipiku, huku zikiwa zimebakia mechi nne ligi hiyo kufikia mwisho.

Wakati sherehe zikiendelea jijini Milan, Hakimi alizungumzia kuhusu Madrid, ambako raia huyo wa Morocco alichomoza kutoka timu ya vijana mwaka 2017 na kucheza mechi 17 kabla ya kutumia miaka miwili kwa mkopo kule Borussia Dortmund na baadaye kupelekwa Inter.

"Real Madrid kulikuwa nyumbani," alisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, akiiambia El Chiringuito.

"Nilipenda kubakia kule na kupambania namba... lakini klabu iliamua vinginevyo.

"Siwezi kumlaumu (kocha mkuu Zinedine) Zidane au bodi. Nafikiri Real Madrid walikuwa na haki juu ya majaliwa yangu."

Hakimi amefunga mabao saba kwenye Serie A katika msimu wake wa kwanza hapo Inter, huku akitoa pasi za mwisho sita chini ya Antonio Conte.





# *Messi afunga bao la 50 la mpira uliokufa Barca*

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi alifunga bao lake la 50 la mpira wa adhabu ndogo ['mpira uliokufa'] katika maisha yake ya soka pale Barcelona wakati akirudisha tena timu hiyo kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Mabao mawili ya Messi kwenye ushindi wa 3-2 dhidi ya Valencia Jumapili, kulimfanya kufikisha 28 aliyofunga kwenye Ligi Kuu msimu huu.

Na hiyo ina maana kwamba, mshindi huyo mara sita wa Ballon d'Or, amebaki kuwa mbele ya Cristiano Ronaldo kwenye mabao mengi waliyofunga katika Ligi Kuu msimu huu.

Messi anaongoza kwa bao moja dhidi ya Ronaldo aliyefunga mabao 27 kule Juventus katika Ligi Kuu msimu huu.

Lakini wote wawili wanaongozwa kwa mbali na mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski, ambaye hadi sasa amefunga mabao 36 katika ligi kubwa tano Ulaya

Kwa maana hiyo sasa, Barcelona ipo nafasi ya tatu kwenye msimamo ikiwa na pointi sawa na Real Madrid (74) waliopo nafasi ya pili kwenye msimamo wa LaLiga.

Atletico Madrid wanaongoza kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo wakiwa na pointi 76, huku kukiwa kumebakiwa mechi nne ligi hiyo kufikia ukingoni.

# Mashabiki wachafua hewa Man United

**MANCHESTER,** England

MAELFU ya mashabiki wa Manchester United walivamia kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi Jumapili na kusababisha mchezo wao dhidi ya Liverpool kuahirishwa.

Mashabiki hao waliandamana kwa ajili ya kushinikiza mmiliki wa timu hiyo, familia ya Glazers kuiachia timu yao.

Mashabiki walizuia basi la wachezaji kuondoka kwenye Hoteli ya Lowry kwenda uwanjani kwa ajili ya kuvaana na Liverpool, na hivyo mamlaka ya usimamizi wa soka kuamua kuusogeza mbele mchezo huo.

Waliandamana nje ya uwanja huo kwa ajili ya kushinikiza kuondoka kwa Glazers, huku kocha Ole Gunnar Solskjaer akitaka maandamano yao yawe ya amani.

Katika picha za video, mashabiki hao walionekana wakilazimisha kuingia hadi katika eneo la kuchezea wakirusha fataki katika majukwaa huku wakipiga kelele kushinikiza familia hiyo ya Marekani kuachia timu yao.

Fataki hizo pia zilionekana kurushwa katika studio za matangazo za Sky Sports, eneo ambalo alikaa mchambuzi na mchezaji wa zamani wa Liverpool, Jamie Carragher.

Sky Sports ilieleza katika matangazo yake kwamba kamera zao zilikuwa hatarini, kwani zilisukumwa na hata vibendera vya kona na vinasa sauti vingine vilichukuliwa na waandamanaji.

The Manchester Evening News liliripoti kwamba takriban mashabiki 10,000 walikuwa katika kampeni hiyo ya kuwaondoa Glazers, wakati wimbi kubwa la mashabiki likiwachoka wamiliki hao raia wa Marekani.







# SALAH HAJUI CHOCHOTE KUHUSU MKATABA

**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool, Mohamed Salah, amesema hakuna ambaye amemfuata kwa sasa kuzungumza naye kuhusu suala la kuongeza mkataba wake mpya ndani ya klabu hiyo.

Mkataba wa sasa wa Salah hapo Liverpool unatarajiwa kumalizika Juni 2023 na inaonekana kwamba hakuna mpango wa nyota huyo kuongezewa mkataba.

Raia huyo wa Misri amekuwa akihusishwa na mpango wa kujiunga na Barcelona pamoja na Real Madrid tangu msimu uliopita.

Lakini katika mahojiano yake na BT Sport, Salah amesema hakuna ambaye amemfuata kuzungumza naye kuhusu suala la mkataba wake jambo ambalo hawezi kulizungumzia kwa sasa.

"Hakuna ambaye anazungumza na mimi kuhusu mkataba, hivyo siwezi kusema zaidi," alisema Salah.

"Tusubiri na tuone, muda utazungumza kwa kuwa mimi sijui lolote lile."

Salah alitua Liverpool mwaka 2017 na amefanikiwa kutwaa taji la Ligi Kuu England, Ligi ya Mabingwa Ulaya na akiwa ni mfungaji bora wa ligi mara mbili.

# *Matumaini ubingwa kumbakisha Conte*

**MILAN,** Italia

OFISA Mtendaji wa Inter Milan, Giuseppe Marotta ana matumaini Antonio Conte atabakia pale San Siro baada ya kuwaongoza 'Nerazzurri' hao kutwaa taji la Serie A kwa mara ya kwanza baada ya kipindi cha miaka 11.

Sare ya bao 1-1 ya Atalanta dhidi ya Sassuolo Jumapili ilimaanisha Inter walitawazwa kuwa mabingwa wapya wa Italia kwa mara ya kwanza tangu Jose Mourinho aliposhinda mataji matatu msimu wa 2009-10.

Pia ilimaliza utawala wa miaka tisa mfululizo kwa Juventus kutwaa taji hilo, matatu kati yake walishinda chini ya Conte wakati akiinoa klabu hiyo kati ya mwaka 2011 na 2014.

Huku mechi nne zikiwa zimebakia kabla ya ligi hiyo kufikia mwisho, Inter inaongoza kileleni mwa msimamo kwa pointi 13 zaidi.

Hata hivyo, majaliwa ya Conte yaliibuka mjadala hapo Inter kutokana na mlipuko wa virusi vya corona huku wamiliki wa klabu hiyo, Suning Holdings Group wakiripotiwa kufikiria kuiuza.

Lakini Marotta - ambaye alifanya kazi na Conte kule Juve - aliiambia Rai: "Mawazo ya Conte ni kama yetu, kufurahia wakati huu. Inter ilihitaji wakati wa furaha, huu ni wakati wa kufurahia kwa kile tulichofanikiwa.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# LEWANDOWSKI MGUU SAWA KUKIPIGA EPL

●●● Kwa sasa amebakisha mkataba wa mwaka mmoja na Bayern na hakuna mazungumzo...

**MUNICH,** Ujerumani

JARIDA la SportBild limeripoti kwamba, uhamisho unaofuata wa mshambuliaji wa Bayern Munich, Robert Lewandowski ni kwenda Ligi Kuu England, EPL.

Ripoti hiyo imesema kuwa kama Bayern itataka kumuuza mchezaji huyo raia wa Poland, basi kituo chake kitakachofuata ni England.

Majaliwa ya Lewandowski kule Bayern yako shakani baada ya uvumi kubainisha kuwa mchezaji huyo hana mpango wa kuongeza mkataba kwa miamba hao wa 'Baravia'.

**Manchester City na Chelsea zinafahamia kwamba, zinataka kuimarisha safu zao za ushambuliaji, hivyo Lewandowski anaweza kufiti katika klabu hizo.**

Ripoti hiyo imedai kuwa wakala wa Lewandowski, Pini Zahavi anajaribu kuwahamasisha Bayern kumwongeza mkataba mpya mnono zaidi mshambuliaji huyo au kumuuza kwenye klabu zenye nguvu ya fedha nchini England.

Lewandowski amebakisha mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa sasa na Bayern, lakini miamba hao wanaonekana kama vile hawana mpango wa kuanzisha mazungumzo ya mkataba mpya.

## ZISIKUPITE

### NEYMAR HAKIELEWEKI PSG

MKURUGENZI wa Michezo wa Paris St-Germain, Leonardo haonekani kushawishika kuwa mshambuliaji wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 29, atasaini nyongeza ya mkataba na klabu hiyo ya Ufaransa. ***(Marca)***

### MOYES AMTAKA ABRAHAM

KOCHA wa West Ham, David Moyes, amesema timu yake itaingia sokoni kumsaka mshambuliaji katika dirisha lijalo la usajili, lakini hawatamwania, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23 endapo bei yake itabakia kuwa pauni milioni 45. ***(Football London)***

### GUARDIOLA ATIA NENO CITY

MANCHESTER City haitakua "sehemu sahihi ya wachezaji" iwapo hawatapata nafasi ya kucheza kila mmoja, hii ni kwa mujibu wa kocha, Pep Guardiola. ***(Manchester Evening News)***

### MILAN NA MIKATABA

MKURUGENZI wa Ufundi wa AC Milan, Paulo Maldini, amesema klabu hiyo itasitisha mazungumzo na wachezaji kuhusu ongezeko la mkataba, baada ya ripoti kuwa, mlinda mlango wa Italia, Gianluigi Donnarumma, ambaye mkataba wake unamalizika msimu huu wa majira ya joto, kukabiliwa na mashabiki. ***(Ansa, via Mail)***

### KANE, GREALISH KWA UNITED

KIUNGO wa kati wa zamani wa Manchester United, Roy Kean, anaamini kuwa klabu hiyo inapaswa kujaribu kumsajili mshambuliaji wa Tottenham, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 na Jack Grealish, 26, anayekipiga kule Aston Villa. ***(Sky Sports)***

### KLOPP AMPA TANO KEITA

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema anaona mustakabali mzuri siku za usoni kwa kiungo, Naby Keita mwenye umri wa miaka 26, katika klabu hiyo. ***(Mail)***

### VARANDA ATAKIWA SPURS

TOTTENHAM Hotspur wanamwinda winga wa Brazil, Rodrigo Varanda na mazungumzo ya awali yameanza ya kumnasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18 anayekipiga Corothians. ***(Sun)***

### ALABA KULIPWA EURO MIL. 12

MLINZI wa kati wa Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, atapokea mshahara wa Euro milioni 12 sawa na mlinzi wa kati wa Real Madrid, Sergio Ramos akitua pale kwenye dimba la Bernabeu kwa uhamisho huru, mara mkataba wake na Bayern Munich utakapomalizika. ***(Fabrizio Romano, via AS)***

### DEMBELE ATAKIWA FULHAM

KLABU ya Fulham inamfuatilia mshambuliaji wa Peterborough United, Siriki Dembele mwenye umri wa miaka 24, ambaye pia anazivutia klabu za Rangers, Celtic na Crysta Palace. ***(Football Insider)***

HABARI MICHEZO

# HITIMANA ATOA SABABU NAMUNGO KUWIKA BARA

**Na Saada Akida**

KIPA namba moja wa Namungo FC, Jonathan Hitimana, amesema michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika (CAF), imewapa uzoefu mkubwa na kuendelea kufanya vizuri katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya Azam Sports Federation Cup (ASFC) maarufu FA Cup.

Namungo juzi ilitinga hatua ya robo fainali ya ASFC baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya JKT Tanzania katika mchezo wa hatua ya 16-bora ya michuano hiyo iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri mjini Morogoro.

Akizungumza na gazeti hili jana, Jonathan alisema michuano ya kimataifa imewapa somo na ukomavu mkubwa wa kupambana kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyokuwa mbele yao ikiwa ni pamoja na kufanya vizuri kwenye Kombe la FA.

Alisema malengo makubwa kwao ni kuhakikisha wanafanya vizuri ili kupata tiketi ya kushiriki tena michuano ya kimataifa msimu ujao.

"Msimu huu tuliondolewa katika hatua ya makundi, ila tumejifunga vitu na kujifunza na sasa tunapambana kufanya vizuri katika michuano ya ASFC hasa katika hatua hii ya robo hadi kucheza fainali kwa sababu ya kutafuta nafasi ya kuiwakilisha nchini," alisema Hitimana. Alisema wamefanikiwa kutinga robo fainali ya ASFC na sasa wanasubiri kuona mpinzani wao watakayecheza naye katika hatua hiyo, lakini wanahitaji kutafuta matokeo mazuri kwenye michezo ya ligi ili kuendelea kubaki kwa msimu ujao.

"Tukiwa tunapambana kutafuta kusonga mbele kwenye ASFC, lakini tunahitaji kupambana kuhakikisha timu inaendelea kubaki kucheza ligi kwa msimu ujao wa ligi hiyo, ambayo imekuwa na ushindani mkubwa kwa sababu kuna timu ambazo zinahitaji ubingwa na za kujiondoa kwenye nafasi ya chini kama ilivyo kwetu," alisema kipa huyo ambaye msimu uliopita alidaki KMC FC.



Waogeleaji wa Tanzania kutoka kushoto, Hilal Hilal, Austin Okore na Collins Saliboko wakiwa nchini Afrika Kusini tayari kwa mafunzo ya kuogelea ya Shirikisho la Mchezo wa Kuogelea la Afrika (Cana) na baadaye Mei 7 na 8, mwaka huu kushindana kuwania nafasi ya kufuzu mashindano ya Olimpiki. **MPIGAPICHA WETU**

## Waogeleaji wapata udhamini kusaka tiketi ya Olimpiki

**Na Mwandishi wetu**

KAMPUNI ya Greatlakes Freight & Transport, imepiga tafu waogeleaji wa Tanzania wanaowania nafasi ya kufuzu mashindano ya Olimpiki yaliyopangwa kufanyika mjini Tokyo, Japan kuanzia Julai 23 hadi Agosti 8, mwaka huu.

Waogeleaji hao wawili, Collins Saliboko na Hilal Hilal, wamechagulia na Chama cha Kuogelea Tanzania (TSA), kusaka tiketi ya kuwania kufuzu mashindano ya Olimpiki yaliyopangwa kufanyika Mei 7 na 8 mjini Stellenbosch, Afrika Kusini.

Wakati Collins amedhaminiwa kuanzia mazoezi ya gym na kwenye maji, Hilal ambaye alikuwa mazoezini Dubai, amedhaminiwa tiketi ya kwenda Afrika Kusini kushiriki katika mashindano hayo na iwapo watafuzu, waogeleaji hao watashiriki katika mashindano hayo ya Tokyo.

Mkurugenzi Mkuu wa Greatlakes Freight & Transport, Fahmy Ahmed, alisema jana kuwa wameamua kusaidia mchezo wa kuogelea ili kuleta hamasa katika mchezo huo na maendeleo kwa vijana.

Fahmy alisema wamedhamini waogeleaji hao kama sehemu ya kampuni kujihusisha na shughuli za kijamii, kuendeleza vipaji vya vijana wa leo na kuhamasisha mchezo huo.

Pia wanahamasisha kampuni nyingine kuwaunga mkono vijana wetu, ili waweze kupeperusha bendera ya Tanzania bila vikwazo na mawazo yanayoweza sababishwa na upungufu wa mazoezi na vifaa stahiki.

Alisema mchezo wa kuogelea una vipaji vingi nchini na pia unatazamwa zaidi katika mashindano ya Olimpiki.

Alisema kwa hapa nchini, mchezo huo unashindwa kuendelea kutokana na kukosa sapoti kutoka kwa jamii na hasa udhamini.

"Kampuni nyingi zinapendelea zaidi kudhamini michezo maarufu, kama mpira wa miguu na ngumi na kuona mchezo wa kuogelea hauna tija na wala haufahamiki," alisema.

Aidha, amewashauri watu kuweka bidii kwenye mchezo huo kwa kuwa una waogeleaji wengi ambao wanaweza kuitangaza nchi nje ya mipaka yake.

Kwa upande wa Makamu Mwenyekiti wa TSA, Asmah Hilal, aliipongeza kampuni hiyo kwa msaada mkubwa na kuwawezesha waogeleaji hao kujiandaa na kwenda kushindana kuwania nafasi ya kufuzu Olimpiki.

Asmah pia alitoa shukrani kwa Kamati ya Olimpiki Tanzania (TOC) na duka la kuuza vifaa vya michezo la Just Fit kwa kusaidia waogeleaji hao.

## Coastal yakana kumtimua Mgunda

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imekanusha taarifa zilizozagaa kuanzia juzi kwenye mitandao ya kijamii kuwa imemfuta kazi kocha wake mkuu, Juma Mgunda kutokana na matokeo mabovu ya timu hiyo.

Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Rashid Mgweno, ameeleza kushangazwa na taarifa hizo na kuongeza wao kama viongozi hawajawaza ama kufikiria jambo hilo kutokana na kocha huyo alivyo ndani ya klabu hiyo.

"Tunazikanusha, hazina ukweli wowote, ni taarifa za uongo. Hatujui zimetokea wapi, lakini tunaendelea kuzifuatilia ili tuchukue hatua kwa sababu zimezua taharuki kwa wanachama na mashabiki wetu, sisi viongozi hata na mwenyewe pia," alisema katibu huyo.

Alisema kuwa Mgunda kwenye klabu ya Coastal si kocha tu kama watu wanavyoona kwa nje, lakini amekuwa zaidi ya kocha, kwani kuna vitu amekuwa akiisaidia klabu hiyo kwenye kuisogeza mbele kupata mafanikio.

"Sisi hatumchukulii kama ni kocha, bali ni kiongozi pia, wakati mwingine anafanya majukumu ambayo si ya kiualimu, bali kama kiongozi ambavyo watu wengi hawaelewi ndiyo maana sisi viongozi hatujawahi hata kuwaza kumfukuza, kwa sababu tunajua na tumfahamu," alisema.

## Yanga kula sahani moja na Asukile

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema itachukua hatua kali kwa mchezaji Benjamin Asukile, endapo akishindwa kuthibitisha madai yake kuwa kuna baadhi ya viongozi waliowapigia simu baadhi ya wachezaji wa Tanzania Prisons kwa madai ya kutaka kutoa pesa kiasi cha Sh. milioni 40 ili wacheze chini ya kiwango kwenye mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la FA lililochezwa Ijumaa iliyopita katika Uwanja wa Nelson Mandela mjini Sumbawanga na wa 'Wajelajela' hao kupigwa bao 1-0.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, amesema kuanzia jana walikuwa kwenye harakati za kuziandikia mamlaka husika kutaka mchezaji huyo ahojiwe na apeleke ushahidi ili hatua zichukuliwe kama kuna baadhi ya watu walihusika na hilo na kama alikuwa anaongea kwa kuichafua klabu ya Yanga, basi watachukua hatua za kisheria dhidi yake.

"Sisi tumemsikia, ni kauli inayoelekea kuichafua klabu yetu ya Yanga, anataka kuonyesha kuwa sisi tusingeweza kuishinda timu yao bila kuwatafuta. Yaani timu yao ni bora sana kuliko Yanga? Wao walifungwa na Ihefu hivi karibuni kwani walihongwa? Yanga ina unyonge gani wa kushindwa kuifunga Prisons?" Alihoji Bumbuli.

# Michezo

Jumanne Mei 4, 2021


Nipashe



LEWANDOWSKI MGUU SAWA KUKIPIGA EPL

HABARI UK 22

TUJIKUMBUSHE...




Winga wa Simba, Luis Miquissone, akipenya na mpira katikati ya mawinga wa Yanga, Tuisila Kisinda (Kulia) na Farid Musa kwenye mechi ya watani wa jadi mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kumalizika kwa sare ya bao 1-1, timu hizo zitakutana tena Jumamosi uwanjani hapo. PICHA: MAKTABA YETU

# Miquissone azua hofu Yanga, Morrison aililia

●●●Asema mbona siku hazifiki mapema, Ninja yeye adai hajamsoma vizuri lakini...

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI zikiwa zimesalia siku nne kabla ya kushuhudiwa mechi kali ya watani wa jadi nchini, Simba na Yanga, tayari homa ya mtanange huo imezidi kupanda baada ya wachezaji wa pande zote kuonyesha kuutamani mchezo huo utakaopigwa Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Kinachoonekana kwa sasa ni wachezaji kuanza kusomana, ambapo beki kisiki wa Yanga, Abdalla Shaibu 'Ninja', ambaye inaaminika ataiongoza safu ya ulinzi ya timu yake, amesema anawafahamu vema wachezaji wa Simba kutokana na kucheza nao mara kadhaa, isipokuwa winga wao, Luis Miquissone.

Ninja amesema anatambua kwamba Simba ina wachezaji ambao ni wasumbufu ila bahati nzuri ni kwamba amewahi kukutana nao uwanjani na anazijua vema mbinu zao.

"Labda mmoja bado, ambaye ni Luis [Miquissone], lakini naye pia ninajua namna anavyocheza, hivyo ni suala la kuomba uzima ili kila kitu kiwe sawa," alisema Ninja anayeaminika kuwa na uwezo mkubwa wa kuwakaba washambuliaji machachari.

Lakini wakati Ninja akieleza hayo, kiungo mnyumbulifu wa timu hiyo, Mnyarwanda Haruna Niyonzima, ambaye amewahi kuichezea Simba, alisema wataingia uwanjani kwa tahadhari kubwa katika mchezo huo kutokana na ubora wa wapinzani wao kwa sasa.

Niyonzima amesema mchezo huo ni muhimu kwao kwani wanahitaji matokeo zaidi ya wapinzani wao ili kurudi katika mbio za kulisaka taji la Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Mchezo wetu dhidi ya Simba mara nyingi huwa mgumu sana, lakini tutaingia kwa tahadhari," alisema.

Kwa upande wa winga wa Simba, Mghana Bernard Morrison, ambaye anapigiwa chapuo na mashabiki wa timu hiyo wakitaka Kocha Mkuu, Mfaransa Didier Gomes kumpa nafasi ya kuanza Jumamosi, ameonyesha kuitamani siku hiyo ifike mapema.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Morrison akionyesha kuitamani mechi hiyo, ameandika: "Bona [mbona] siku haziendi. Nimesahau tarehe."

Morrison alionyesha kiwango cha juu katika mechi ya hatua ya 16-bora ya Kombe la FA Jumamosi, baada ya kuingia kipindi cha pili akitokea benchi wakati huo Simba ikiwa imelala bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar na kuisawazishia kisha kumtengenezea bao la ushindi Meddie Kagere na kuifanya timu yake kuibuka na ushindi wa mabao 2-1.

Lakini Didier Gomes, alipoulizwa nafasi ya Morrison kuanza Jumamosi alisema: "Tutaona, Morrison ni mchezaji maalum, ana uwezo wa kuamua mechi, ni muhimu. Yeye ni mchezaji huru, lazima tuzibe nafasi anapokuwa uwanjani.

"Unajua dhidi ya Yanga ni jambo lingine na Morrison ni aina ya wachezaji wazuri ambao wapo kwenye kikosi, kuelekea kwenye mchezo wetu dhidi ya Yanga ni suala la kusubiri mambo yatakuaje kwani bado kuna muda wa kujiandaa." Simba ambayo ipo kileleni mwa msimamo ikiwa na pointi 61, nne mbele ya Yanga iliyopo mbele kwa michezo miwili, katika raundi ya kwanza ya ligi hiyo ililazimisha sare ya bao 1-1 katika uwanja huo.

# KOCHA WA YANGA AAHIDI 3 ZA SIMBA

**Na Saada Akida**

HUKU wakiendelea kukiandaa kikosi chao tayari kwa ajili ya mechi ya watani wa jadi, Kocha Msaidizi wa Yanga, Razak Siwa, amesema hawana hofu juu ya wapinzani wao, Simba, kwani wanachokiwaza ni kupigania malengo yao ya kuvuna pointi tatu katika kila mechi ikiwano hiyo ya Jumamosi.

Simba itaikaribisha Yanga Jumamosi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi ya raundi ya pili baada ya mzunguko wa kwanza timu hizo kutoshana nguvu kwa kutoka sare ya bao 1-1 uwanjani hapo.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Siwa alisema ana imani itakuwa mechi ngumu na ushindani mkubwa kutokana na wapinzani wao kuonekana tishio na bora ila wana imani wako vizuri na tayari kwa ajili ya mchezo huo.

"Nina imani hakuna kitakachoshindikana, tumerejea jijini na kuingia kambini kuendelea na maandalizi yetu kuelekea mchezo huo ambao ni muhimu kwa kila mmoja wetu, kwa upande wetu tunahitaji kupata pointi tatu ili kuendelea kupunguza pointi za mpinzani wetu huyo," alisema Siwa.

Alisema ana imani bado hawajaondoka katika mbio za ubingwa kwa sababu wanahitaji ushindi kwenye mchezo huo ili kujiweka vizuri zaidi katika vita hivyo vya ubingwa.

Kuhusu hali ya Tuisila Kisinda, Siwa alisema anaendelea vizuri na suala la kucheza kwenye mechi hiyo ni jukumu ya Kocha Mkuu, Nasreddine Nabi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002